SUPA JACKPOT
TZS. 1,157,290,273
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Jumamosi Septemba 30, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581449
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Watatu** wafariki katika mapigano wakulima, wafugaji



UKURASA 2

MAHOJIANO MAALUM - 2

**Bosi** mpya CMA na mikakati ya utatuzi migogoro



UKURASA 4

**Uswisi** yaipatia Tanzania bil. 50/-mpango wa TASAF

UKURASA 5



# Simbachawene akemea viongozi miungu watu


UKURASA 2

## CHADEMA yapendekeza katiba mpito kabla uchaguzi

UKURASA 3




UKURASA 11



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga

# TANESCO yapewa kibano kukatika kwa umeme

UKURASA 3

MICHEZO YANGA KAMILI KUVUNJA REKODI UK.24 MAONI UK.6

HABARI KITAIFA




Wafanyabiashara wadogo maarufu machinga wa soko la Tengeru, wakiwa wameandamana na kufunga barabara ya Moshi–Arusha kwa kutumia meza za biashara juzi, wakiishinikiza Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru kuziondoa meza hizo wakipinga kuzilipia 4,000/- kwa siku kwa madai kuwa ni kubwa. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Simbachawene akemea viongozi miungu watu

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amekemea baadhi ya viongozi kujifanya miungu watu

Amesema baadhi ya viongozi wanapopata nafasi wamekuwa wakitumia mamlaka yao kubadilisha watu wakidhani ndio uongozi na wengine wakiwatisha watu kwa kujitambulisha 'unanijua mimi ni nani?

Pia amesema sambamba na watu hao, wako wanaopambana kusaka uongozi kwa ajili ya kulipa visasi kwa watu waliowaumiza ambao bahati mbaya waliowafanyia hivyo, wameshafariki dunia.

Simbachawene aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akifungua mafunzo ya uongozi ngazi ya cheti awamu ya nne yenye washiriki 70 yaliyoandaliwa na Taasisi ya Uongozi.

Alisema kutokana na tabia hiyo, kuna watu wengi ambao hawana majukumu ya kufanya kwa kuwa wanaoongoza hudhani kuwabadilisha watu ndiyo kujua kuongoza.

Simbachawene aliwakumbusha kuwa kuna baadhi ya nafasi ambazo zipo kwa mujibu wa sheria na majukumu yake ni kuendeleza malengo yanayojulikana.

Hata hivyo, Simbachawene alisema siku hizi kumetokea utaratibu wa mtu akifika kwenye ofisi, anaanza kuwaondoa wafanyakazi kwa kisingizio hawaendani na kasi ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Kimsingi ni kwamba anatakа kuwatoa na kuweka marafiki zake. Kiongozi wa namna hiyo akipewa madaraka kwa nafasi yoyote, sizungumzii kiongozi wa kisiasa bali ni yoyote aliye kiongozi anakuwa kikwazo katika uongozi. Sasa unapewaje watu wa kuwaongoza halafu unakwenda kuwaondoa? Sasa ukiwaondoa unabaki na nani? Halafu unaongoza vipi? Matokeo yake unakuta kuna watu wengi wapo bila kuwa na majukumu," alisema.

Simbachawene aliwakumbusha kuwa kiongozi mzuri anatakiwa kuweka maono na mikakati na wafanyakazi hao watabadilika na kwenda na mwelekeo wake badala ya kukimbilia kuwaondoa.

"Hapa sipo kwa ajili ya kuwafundisha ila hili eneo mlifanyie kazi na mpate uelewa kwa maana ya kwenda kuongoza si uongozi wa kwenda kuchukua madaraka na kuanza kufyetua fyetua watu na kujiona wewe ndiwe kiongozi. Kiongozi ni yule ambaye anakwenda kubadilisha watu kimtazamo na kifikra na si kuwaondoa.

"Juzi, nilipokuwa ninaongea na viongozi kule Dodoma tuliunganisha wadau wanaosimamia maadili. Nilitoa kauli ambayo ilikuwa kidogo ngumu kwamba unapoteuliwa kuwa kiongozi kwenye eneo, matarajio ya aliyekupa nafasi ya kuongoza ni kuona unawabadilisha unaokwenda kuwakuta na kuwa na mwelekeo wa maelekezo uliyoyapata," alisema.

Simbachawene alisema wataendelea kushirikiana na wadau wengine kusimamia maelekezo ya serikali ili kuhakikisha viongozi wote na watendaji wanapata mafunzo ya uongozi ili kuongeza uwezo na kuimarika katika nyanja muhimu za utendaji kazi.

Alisema mafunzo hayo yatasaidia kuwa na mbinu mpya za kukabiliana na changamoto katika kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo huku akiwakumbusha kwamba misingi ipo mitatu inayotakiwa kuzingatiwa ambayo ni kufuata sheria, maadili na haki.

Program hizo za uongozi, alisema zinalenga kuimarisha uwezo kwa viongozi katika maeneo matatu ambayo ni usimamizi wa taasisi au mashirika, kuongoza rasilimali watu na kujenga sifa binafsi za kiongozi. "Ukiona kiongozi anayeanza kusema 'unanijua mimi ni nani?' unataka kujitambulisha kuwa wewe ni kiongozi. Kiongozi hutakiwi kujulikana, ukianza kusema 'mimi ni nani?' maana yake umeshindwa. Kiongozi anajulikana kwa namna ya mwonekano, atakavyozungumza, anavyosimamia, maadili, heshima na tabia ya kupenda kusimamia haki,"alikumbusha.

Simbachawene alisema kuna watu ambao wanapambana kutaka uongozi kwa ajili ya kulipa kisasi kwa watu waliowaumiza ambao bahati mbaya waliowafanyia hivyo, wameshafariki.

"Sasa unataka kuwaumiza wengine ambao hawahusiki na changamoto ulizozipata. Kiongozi mzuri anajitambulisha kwa namna alivyo na si yeye. Programu hii itasaidia kutekeleza misingi niliyoieleza na imani mkirudi huko kutatokea utofauti," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Kadari Singo, alisema wana jukumu kubwa la kuwaandaa na kuendesha mafunzo kwa viongozi ili wawe bora na wenye maadili.

Alisema programu ya uongozi ngazi ya cheti awamu ya nne ambayo itaendeshwa kwa muda wa miezi sita ni muhimu, kwani ina lengo la kuwajengea uwezo viongozi kuwa bora katika kutekeleza majukumu yao.

Alisema Taasisi ya Uongozi itaendelea kutoa ushauri wa kitalaam na kuzisaidia taasisi mbalimbali na viongozi wake katika kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Balozi wa Finland, Theresa Zitting, alisema kwa muda mrefu wamekuwa na uhusiano mzuri na Tanzania na kwamba, mafunzo hayo yatasaidia viongozi hao kufanya kazi zao kwa uweledi na kuongeza tija.

# Watatu wafariki katika mapigano wakulima, wafugaji

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANAUME watatu wakazi wa vijiji vya Matekwe,Nachingwea mkoani Lindi na Tinginya wilaya ya Tunduru, mkoa wa Ruvuma, wamefariki dunia baada ya kuibuka upya mapigano kati ya wafugaji na wakulima.

Taarifa kutoka katika vijiji hivyo zilizothibitishwa na Jeshi la Polisi, zilisema vurugu hizo zilitokea Septemba 23, mwaka huu, mchana na kutokana na mapigano hayo, diwani anashikiliwa.

Waliofariki dunia katika mapigano hayo ni Kidabelega Longoda (31), Nyerere Kisingwenga (80) ambao ni wafugaji waliopangiwa kuishi na kufuga kijiji cha Matekwe na Fadhili Abdallah (33) mkulima wa kijiji cha Tinginya.

Wakizungumzia kwa sharti la kutotajwa majina, baadhi ya mashuhuda wametaja chanzo cha vurugu hizo ni wafugaji kupeleka mifugo yao katika shamba la Fadhili Abdallah kwa ajili ya malisho.

Mashuhuda hao walisema mkulima huyo alipohoji sababu za wafugaji kulisha ng'ombe wao kwenye shamba lake, ndipo alipopata kipigo kilichosababisha kupoteza maisha.

Kwa mujibu wa mashuhuda hao, hali hiyo iliibua hasira kutoka kwa wananchi wengine na kwenda kujibu mashambulizi kwa wafugaji.

"Wanakijiji baada ya kuona mwenzao amepigwa na kuuawa walichukua uamuzi wa kuwafuata wafugaji waliohusika na kuwapiga na kusababisha vifo vya watu wawili," walisimulia.

Walisema kutokana na vurugu hizo, kamati za ulinzi na usalama kutoka Nachingwea na Tunduru, zikiongozwa na wakuu wa wilaya hizo, zilifika eneo la tukio.

Wakuu wa Wilaya, Mohamedi Moyo (Nachingwea) na Julius Mtatiro (Tunduru) wakizungumza na wananchi wa vijiji hivyo, waliwataka waendelee kuishi kwa amani na upendo bila kufanya vurugu.

"Tunachopenda kuwaambieni mwendelee kuishi kwa amani, ikizingatiwa nyinyi mnaishi mpakani mwa Wilaya za Nachingwea na Tunduru," Walisema viongozi hao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Pili Mande, alisema wanamshikilia Diwani wa Tinginya, Tunduru, Eliasa Msahani (45), kwa madai ya kuwashawishi wananchi kulipiza kisasi cha mauaji kwa wafugaji pamoja na kuharibu mali kwa kuzichoma moto.

Mande alitaja baadhi ya mali za wafugaji zilizoteketezwa kwa kuchoma moto ni pamoja na vibanda 15 walivyokuwa wakiishi.

HABARI KITAIFA




Mkurugenzi wa Wakala wa Elimu Vyuo Vikuu Global Education Link (GEL), Abdulmalick Mollel akizungumza na wazazi na wanafunzi wanaotarajiwa kusafiri kwenda nje ya nchi kwa masomo kupitia taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TANESCO yapewa kibano kukatika umeme

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, ametoa saa mbili kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kutatua tatizo la kukatika kwa umeme katika kituo cha uzalishaji umeme cha Ubungo One, Dar es Salaam.

Kapinga alitoa maagizo hayo jana alipotembelea makao makuu ya shirika hilo yaliyoko Ubungo kwa ajili ya kukagua hali ya uzalishaji wa umeme katika vituo vya Ubungo One na Ubungo Two.

Baada ya kutembelea vituo hivyo, Kapinga alisema kwenye kituo cha Ubungo Two mashine za kuzalisha umeme ziko tatu lakini moja haifanyi kazi na iko kwenye matengenezo, zote zikiwa na uwezo wa kuzalisha megawati 43 kila moja.

Alisema kwenye kituo cha Ubungo One, mashine ziko 12 lakini sita kati ya hizo ziko kwenye matengenezo na kwamba muda wowote zitakamilika na kurejesha uzalishaji kama awali.

"Kutokana na hali hii na namna tulivyo na changamoto ya umeme kwa sasa, nimewaelekeza TANESCO wahakikishe wanakuwa na mpango madhubuti wa kufanya marekebisho kwa muda mfupi.

"Yale matengenezo yanayochukua muda mfupi yafanyike kwa muda mfupi na yakamilike kwa wakati na yale yanayochukua muda mrefu yakamilike kwa wakati," aliagiza.

Kapinga alisema adhma ya serikali ni kuona Watanzania wanapata umeme na kukamilisha matengenezo hayo ndani ya miezi sita.

Alisema kama marekebisho hayo yatafanyika kwa wakati tatizo la umeme litakwisha.

"Kituo cha Ubungo One kimekatika umeme na nimewaagiza TANESCO ndani ya saa mbili umeme urejee na kama itashindikana ndani muda huo, ndani ya saa sita watumie mbinu mbadala kuhakikisha umeme unapatikana.

"Hizo mashine sita zilizoharibika zinalisha megawati 42 na 43. Wataalamu wako wanahangaika kurejesha. Ninaamini baada ya marekebisho hayo tatizo litakuwa limekwisha," alisema.

# DPP awaonya wahalifu, asema hawako salama

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, ametoa onyo kwa wahalifu wote walioko kwenye mipaka na ndani ya nchi kuwa hawako salama na kamwe hawataachwa.

Mwakitalu alisema hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha tathmini cha menejimenti, wakuu wa mashtaka, wakuu wa taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa mikoa na wakuu wa upelelezi mikoa kilichofanyika jijini hapa.

Alisema kuwa vitendo hivyo vya uhalifu vimekuwa vikileta madhara makubwa kama vile ya ufisadi na rushwa kwa jamii na kusababisha wananchi kukosa huduma wanazozitaka.

Alisema vikao kama hivyo vinasaidia kwa kiasi kikubwa kutafuta suluhu ya changamoto zinazojitokeza katika jamii hususani katika makosa ya uhalifu, ufisadi na rushwa.

Mkurugenzi huyo pia aliwataka kufanya kazi kwa maslahi ya kuwasaidia wananchi kupata haki zao za msingi.

Amewataka wakuu hao kuweka kipaumbele mapambano dhidi ya uhalifu wowote unaojitokeza ukiwamo ufisadi, rushwa na uhujumu uchumi kwa kuwa umekuwa ukirudisha nyuma maendeleo ya nchi na wananchi kwa ujumla.

"Ili kufanikisha mnatakiwa kuungana kwa pamoja kwa kufanya kazi kwa kushirikiana na hapo mtaona mafanikio katika kukomesha maovu hayo," alisema.

Alisema wakifanya kazi kwa pamoja na kwa kushirikiana, watafanikiwa kukomesha uhalifu na wataweza kuwasaidia wananchi kwa kuwatendea haki zao kimsingi badala ya kila mmoja wapo kufanya kivyake.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi za Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Salumu Hamduni, alisema kuwa wataendelea kushirikiana kwa pamoja ili haki, amani na usalama ipatikane katika jamii.

Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Kamishana (CP) Ramadhani Kingai, alisema ushirikiano ni jambo muhimu katika kuwatendea haki wananchi kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo ndani ya nchi.

# CHADEMA yapendekeza katiba mpito kabla uchaguzi

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, amesema kama serikali haiko tayari kuharakisha mchakato wa Katiba Mpya, ifanye marekebisho ya Katiba ya mpito ili kushughulikia masuala ya uchaguzi kuwa huru na wa haki.

Mnyika aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akifungua kikao cha mafunzo cha Baraza la Wanawake Chadema (BAWACHA) kilichokuwa kikijadili mada mbalimbali.

Mnyika alisema katiba inapaswa kurekebishwa na sheria zote ziendane na marekebisho hayo ili nchi inapoingia kwenye uchaguzi kuanzia wa serikali za mitaa mwakani, kuruhusu Tume ya Taifa Uchaguzi (NEC) isimamie.

"Nitoe wito kwa serikali kwa Rais na wadau wa demokrasia kinachotakiwa kufanyika katika taifa letu kwa sasa kwa haraka ni mambo matatu. Moja, kupelekwa bungeni muswada wa sheria wa kuendeleza mchakato wa katiba ili tuianze safari ya kupata katiba mpya katika taifa letu," alisisitiza.

Mnyika alitaja jambo la pili ni kupeleka bungeni muswada wa sheria ya marekebisho ya katiba ya mwaka 1977, ili safari ya katiba mpya kutokana na kucheleweshwa kwa watawala wanapokwenda kwenye uchaguzi iwe imefanyiwa marekebisho yanayohusu uchaguzi.

Alisema, hiyo itawezesha kuweka mazingira ya kuwa na uchaguzi huru na haki ikiwamo wakurugenzi kuondolewa kusimamia uchaguzi.

Jambo la tatu, alisema ni kupelekwa kwa miswada ya sheria kwa kuwa hawawezi kupeleka miswada inayopingana na katiba, lazima irekebishwe mifumo ya katiba ndipo sheria zitengenezwe. Mnyika alisema awali kulikuwa na matumaini makubwa kwamba Rais Samia Suluhu Hassan ataanzisha mchakato wa katiba lakini baada ya miezi michache, matumaini hayo yakavurugwa. Alisema baada ya Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, kukamatwa taifa likawa halizungumzi tena mchakato wa katiba na kujikuta wanatumia muda mwingi kukimbizana mahakamani kutafuta haki.

Mnyika alisema Mbowe baada ya kutoka alikutana na Rais Samia wakaanza mazungumzo na kuonyesha matumaini ya kuanza kwa mchakato wa katiba.

"CCM nao walikubali mchakato wa katiba uendelee. Ilikuwa Julai 22, 2022 na tulikuwa na matumaini ya maneno, hapakuwa na matendo. Ikafika Desemba tukawakumbusha mbona tumekwama? ilipofika Januari, mwaka huu, Rais Samia akaondoa zuio la mikutano ya hadhara na kuahidi kuunda kamati ya kuendelea na mchakato wa Katiba mpya.

"Rais alitamka kwamba inabidi wananchi wapewe elimu ya katiba ndiyo mchakato uendelee. Kwa msingi huo, ina maana Rais ametupiga kauli ambayo ilikuwa imetolewa na Waziri wa Katiba na Sheria kwamba, Watanzania wapatiwe elimu ya katiba kwa miaka mitatu jambo ambalo haliwezi kukubalika," alisema.

Mnyika aliitaka BAWACHA kujadili kauli hiyo na kuja na tamko lao kuhusiana na suala hilo.

Alisema, Rais alieleza anakusudia kuunda kamati kuhusu mchakato wa katiba na kwamba atavialika vyama kuwasilisha wajumbe, ingawa hakuongea chochote kupeleka bungeni muswada wa sheria utakaoweka utaratibu wa kuendeleza mchakato wa katiba.

"Matatizo mengi yanaanzia kwenye katiba ikiwamo muundo wa tume, katiba inazuia matokeo ya Rais kupingwa mahakamani, inazuia mgombea binafsi, katiba inafanya wanawake wasiwe asilimia 50 kwa 50 bungeni kwa sababu ya muundo wa katiba," alibainisha.

MAKALA MAALUM -2

# Bosi mpya CMA na mikakati utatuzi wa migogoro ya kazi

**Katika sehemu ya kwanza ya mahojiano maalumu, Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Usekelege Mopulla, alifichua siri kuhusu uteuzi wake. Katika sehemu hii ya pili na ya mwisho, anaelezea mikakati yake katika kupunguza mashauri ya migogoro ya kazi...**



Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Usekelege Mopulla.

**SWALI: Awali ulieleza ulivyofanikisha usuluhishi wa migogoro ya kazi ulipokuwa Tanga na Dar es Salaam na sasa umekuwa. Je, utatumiaje uzoefu wako ili kuleta matokeo makubwa kitaifa?**

**JIBU:** Kama nilivyosema awali, migogoro ya kazi inaathiri ukuaji wa uchumi, hivyo kupungua kwake kunachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wake hasa katika uzalishaji mali. Katika kuliendea jukumu hili, natambua lengo la serikali ni kuendelea kukuza uchumi ili kufikia uchumi wa kati unaotokana na maendeleo ya viwanda.

Kwa hiyo katika kutekeleza jukumu hili kubwa, tunapaswa kwenda na kauli ya mkuu wa nchi kuhusu zile R nne. Kwa CMA, ili kufikia malengo ya kukuza uchumi, mkakati ni kuboresha huduma za usuluhishi na kumaliza migogoro kwa muda mfupi. Usuluhishi ndiyo nguzo kubwa katika kumaliza migogoro kwa haraka pasipo gharama kubwa.

Jambo lingine ni kuboreha mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi. Kubwa zaidi, maono katika kufikia malengo ni kuboresha huduma kwa wananchi. Kwa mfano, katika viwanda, CMA iwe na usuluhishi unaotembea, yaani kunakuwa na magari yanayofuata migogoro maeneo husika ambayo CMA haina ofisi. Mfano katika mkoa wa Morogoro, maeneo kama Ulanga, Kilosa na Malinyi hakuna ofisi, hivyo ili kufika huko na kutatua migogoro ya kazi, lazima tuwe na gari na watumishi wanakwenda huko na hatimaye kufanya usuluhishi.

Lakini pia natambua kuwa CMA si kisiwa, kwa maana haifanyi kazi peke yake, hivyo inashirikiana na taasisi zingine. Tunatarajai kuboresha ushirikiano na taasisi zingine kama Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Chama cha Waajiri Tanzania, Ofisi ya Kamishna wa Kazi, taasisi zote chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, vyama vya wafanyakazi, Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) na mifuko ya hifadhi ya jamii. Ushirikiano huu utaboresha utendaji wetu kwa sababu taasisi hizi zitapata mwanga mpana kuhusu CMA na hatimaye kuleta ufanisi.

**SWALI: Nini mkakati wako katika kupunguza mrundikano wa mashauri?**

**JIBU:** Mkakati mkubwa katika hili ni kuondokana na kasumba iliyojengeka kwa baadhi ya watumishi ya 'njoo kesho njoo kesho'. Sheria imeweka ukomo kwamba usuluhishi ufanyike na kumalizika ndani ya siku 30 lakini kwa ndani tumejiwekea siku 21. Hilo tutaliweke mkazo kuhakikisha tunatekeleza malengo kama tulivyojiwekea.

Mfumo wa uongozaji mashauri (case management guide) umetuwezesha kutekeleza majukumu tulivyojiwekea. Mfumo huu unatuwezesha kufuatilia nani anachelewesha mashauri. Kila mtumishi anafuatiliwa namna anavyoendesha mashauri.

Mkakati mwingine ni kuendelea kuwa na kambi za usuluhishi kwa watumishi kupelekwa katika maeneo yenye migogoro na kufanya usuluhishi kwa muda maalum. Pia tuna changamoto ya kuwapo watumishi wacheche, hivyo tutaomba watumishi Zaidi waajiriwe.

**SWALI: Mambo mengi katika utendaji yakifanywa kidijitali. CMA imejipangaje katika hilo?**

**JIBU:** TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) ndiyo mpango mzima katika uendeshaji wa shughuli zote za serikali. Mfumo huu unaondoa utendaji kazi kutoka kwenye makaratasi na unatumia muda mfupi na kwa ufanisi.

CMA ina mfumo unaoongoza katika uendeshaji mashauri, ujulikanao kama 'Case Management Guide'. Kupitia mfumo huu, usajili wa mashauri yanayohusu migogoro ya kazi ni kwa njia ya mtandao. Mtu anasajili mgogoro aliko bila kufika ofisi za CMA. Pia usililizaji mashauri ni kwa njia ya video, wahusika wanakuwa mahali walipo badala ya kuondoka ofisini.

**SWALI: Umezungumzia changamoto za mazingira ya kazi na vitendea kazi. Unaweza kueleza kwa kifupi baadhi ya changamoto hizo?**

**JIBU:** Moja ya changamoto ni waamuzi wawili hadi watatu kutumia ofisi moja. Lengo ni kila mwamuzi awe na ofisi yake. Dar es Salaam kwa mfano, baada ya serikali kuhamia Dodoma, kuna majengo mengi yako wazi, hivyo tutajaribu kuomba serikali iyatoe kwa ajili ya CMA ili kuondoa changamoto hii.

**SWALI: Suala la kifedha kwa taasisi nyingi za serikali ni changamoto na matokeo yake ni kuathiri utekelezaji wa majukumu. Hilo likoje kwa CMA?**

**JIBU:** Kwa ujumla, CMA kwa uendeshaji wake unategemea bajeti ya serikali. Kama kiasi kikubwa, bajeti ya serikali haitoshelezi au kuwezesha kutekeleza kazi za tume.

Kifungu cha 23 cha sheria iliyoanzisha CMA kinaweka vyanzo vya mapato ya tume kwamba ni kutoka serikali kuu, michango kutoka kwa wadau, wahisani na vyanzo vingine bila kuathiri uhuru wake. Zamani tulipata misaada kutoka DANIDA (Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Denmark) na ILO (Shirika la Kazi Duniani).

Kutokana na uwapo wa kifungu hicho, kwa kushirikiana na wenzangu, natarajia kutatatufa fedha kutoka vyanzo vingine. Lakini ikumbukwe kwamba huduma za CMA ni bure, sasa kama ilivyo kwenye vyombo vingine vya sheria kama vile mahakama, tutajaribu kuona kama kuna uwezekano wa kukusanya maduhuli kidogo kwa wadaawa kulipia fedha kidogo wakati wa kufungua mashauri ili kuboresha huduma zetu.

**SWALI: Rushwa ni moja ya mambo yanayolalamikiwa katika vyombo vya utoaji haki. Unalizungumziaje hili na kama litajitokeza ndani ya CMA utachukua hatua gani?**

**JIBU:** Rushwa ni suala mtambuka na ni adui wa haki. Kwangu rushwa ni adui namba moja. Natambua panapokuwa na rushwa haki inapotea. Chini ya uongozi wangu ndani ya CMA, tutafanya kila jitihada kuziba mianya ya rushwa na kutoa huduma kwa weledi na kwa wakati.

Kwa mantiki hiyo, sitasita kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu dhidi ya mtumishi yeyote atakayethibitika kujihusisha na vitendo vya rushwa.

**SWALI: Je, kwa sasa ndani ya CMA kuna mikakati ya kupambana na rushwa?**

**JIBU:** Kwa saa tuna dawati la malalamiko ambalo katika kipindi changu cha uongozi, nitakachofanya ni kuliwezesha. Mtu atakayepewa dhamana ya kulisimamia atwajibika moja kwa moja kwangu.

Aidha, kabla sijateuliwa kuwa Mkurugenzi, nilikuwa mwenyekiti wa masuala ya uadilifu wa taasisi na nilikuwa naripoti kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Awali, nilikuwa makamu mwenyekiti, hivyo kurejea kwa mara ya pili katika jukumu hili, naamini niliaminiwa kuwa nina uadui mkubwa na rushwa.

**SWALI: Awali ulisema moja ya mambo yaliyofanikisha kutatua migogoro ulipokuwa ofisa mfawidhi ni elimu kwa umma. Sasa ukiwa Mkurugenzi wa CMA utatumiaje jukwaa hili katika kuleta ufanisi wa majukumu yako na tume kwa ujumla?**

**JIBU:** Suala hili tutalizingatia sana. Tutatoa elimu kwa umma kuhusu CMA na namna ya utatuzi wa migogoro pamoja na njia za kufuata katika kufanya hivyo. Pia tutashiriki katika hili kupitia vyombo vya habari na matukio ya kitaifa kama vile Sabasaba, Nanenane, Mei Mosi, Wiki ya Sheria na Mbio za Mwenge.

**SWALI: Watu wengi wamekuwa wakishindwa kutofautisha kati ya Mahakama ya Kazi na CMA. Unaweza kueleza tofauti za taasisi hizi?**

**JIBU:** Sheria ya Taasisi za Kazi inaeleza vyombo vinavyoshughulikia masuala au migogoro ya kazi. taasisi hizi ni CMA na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi.

Taasisi zote hizo zinashughulikia migogoro ya kazi lakini tofauti ni kwamba CMA inahusika na migogoro yote inayojitokeza na pindi inapotoa uamuzi wake, mtu asiyeridhika anakwenda Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi. Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi ni ngazi ya rufani kwa uamuzi unaotolewa CMA kama upande mmoja hautaridhika

Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi kazi yake nyingine ni kusikiliza marejeo ya wasioridhika na uamuzi wa CMA. Pia hukazia uamuzi wa CMA ili yule aliyeshinda shauri alipwe tuzo, mali za aliyeshindwa shauri ziuzwe ili kumlipa mhusika au kukamatwa kwa akaunti za benki.

**SWALI: Nini ushauri wako kwa Watanzania kuhusu CMA?**

**JIBU:** Ujumbe wangu kwa Watanzania, weipe ushirikiano CMA. Watambue kwamba lengo letu si kusuluhisha migogoro bali kuchochea ukuaji wa uchumi.

Wale wenye migogoro ya kazi, wasipoteze muda kwenda sehemu zingine badala yake wafike CMA na watumie muda uliopangwa kisheria katika kufungua mashauri yao. Watanzania watambue kuwa CMA ndicho chombo pekee cha kutatua migogoro ya kikazi. Tupo kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania.

HABARI KITAIFA

# Uswisi, Ireland zamwaga bil. 50/-mpango wa kunusuru kaya maskini

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imepokea msaada wa Sh. bilioni 50.13 kutoka Uswisi na Ireland kwa ajili ya Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Awamu ya Pili (PSSNII).

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana baada ya utiaji saini wa mikataba ya fedha hizo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba, alisema kati ya fedha hizo, Dola za Marekani milioni 18 zimetolewa na Uswisi na Dola milioni 2.3 zimetolewa na Ireland.

Dk. Mwamba alisema fedha hizo ni mwendelezo wa misaada iliyokuwa inatolewa na mataifa hayo tangu awali. Awamu ya kwanza, Uswisi ilitoa Dola milioni 17.1 na Ireland Euro milioni mbili. Alisema PSSN II inaendelea na Dira ya Tanzania ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ambayo inatoa mwelekeo wa juhudi za kuleta maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii hadi kufikia mwaka 2025.

Bajeti ya PSSNII, alisema ni Dola za Marekani milioni 883.32 na kwamba matumaini ya serikali ni kufikia malengo yaliyokusudiwa itakapofika Septemba, 2025. "Natoa shukrani zangu za dhati kwa misaada ya wadau wengine wa maendeleo wanaochangia bajeti hii kubwa ya PSSN II. Baadhi yao wamewakilishwa hapa ambao ni Benki ya Dunia (WB), serikali ya Sweden, serikali ya Norway, serikali ya Uingereza, UNICEF na Umoja wa Ulaya (EU). Tunashukuru sana kwa msaada wenu," alisema Dk. Mwamba. Alisema progamu PSSNII inatarajia kuboresha upatikanaji wa fursa za vipato na huduma za kijamii na kiuchumi kwa walengwa ambao ni kaya maskini, pia kuboresha maendeleo ya watoto.

"Pia itaongeza uwezo wa kupata mahitaji muhimu, kaya maskini kupata fursa ya kujihusisha katika shughuli bora za kujipatia kipato, kuongezeka kwa mahudhurio ya watoto wao shuleni na kwenye vituo vya afya," alisema.

Dk. Mwamba alisema TASAF imewezesha wanafunzi kutoka katika kaya maskini kupata elimu ya sekondari na elimu ya juu ambapo mwaka 2022, wanafunzi waliopata asilimia 100 ya mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ni 2,950 chini ya msaada wa PSSN II.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Shedrack Mziray, alisema hadi sasa walengwa milioni 1.3 wamefikiwa pamoja na ruzuku ya Sh. bilioni 7.778 zimetolewa kwa walengwa wa TASAF.

Alisema pia, wamefanikiwa kutoa ajira za muda zaidi ya 660,000 pamoja na kuviwezesha vikundi vya wanawake vya kuweka na kukopa zaidi ya 51,000. Balozi wa Uswiss nchini Tanzania, Didier Chassot, alisema msaada walioutoa ni mwendelezo wa ushirikiano baina ya Tanzania na Uswiss, tangu mwaka 2020 serikali ya Uswisi imekuwa ikitoa misaada katika PSSN .

Balozi wa Ireland nchini Tanzania, Mary O'neil, alisema ushirikiano wa Tanzania na Ireland ni wa zaidi ya miaka 40, kwa kipindi hicho chote wamekuwa wakisaidia katika kuwawezesha wanawake, amani, sera na kaya masikini.




Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (kulia), akikabidhi mfano wa funguo ya gari kwa mjasiriamali wa madini, Nkwimba Anthon wakati wa ufunguzi wa ofisi za kampuni ya GF na kukabidhi magari yaliyonunuliwa wakati wa maonyesho ya madini mkoani Geita mapema wiki hii. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa kampuni ya GF Trucks & Equipment, Salman Karmal. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Achomwa moto hadi kufa madai ya wizi wa ng'ombe

**Na Steven William,** MUHEZA

RAMADHANI Omari (24), mkazi wa mji wa Pongwe jijini Tanga, ameuawa kwa kuchomwa moto na wananchi wenye hasira, akidaiwa kushiriki kuiba ng'ombe na wenzake ambao walikimbia.

Tukio hilo lilitokea juzi alfajiri maeneo ya kijiji cha Tanganyika, Kata ya Lusanga nje kidogo ya mji wa Muheza huku wazazi wa kijana huyo, wakianguka na kupoteza fahamu.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tanga, Almachius Muchunguzi, alisema baada ya wezi hao kuiba ng'ombe huyo kambi ya Kitisa kwa mfugaji Daud Raymond (48), walikwenda kumchinja katika mashamba yaliyoko katika kijiji cha Tanganyika wilayani hapa.

Alisema wakati wezi hao wakibeba nyama, ndipo kundi la wafugaji liliibuka alfajiri hiyo na kuanza kuwasaka baada ya kupeana taarifa kuhusu wizi huo.

Kamanda Muchunguzi alisema wafugaji hao wakati wanawasaka wezi hao waliwakuta kijijini hapo wamemchinja huku kukiwa na ushahidi wa kwato, utumbo na kichwa.

Alisema wezi hao baada ya kuwaona wafugaji, walikimbia na Omari ambaye ni marehemu, aliyekuwa na pikipiki yenye namba MC 907 DXR, alishindwa kukimbia ndipo alivamiwa na kupigwa hadi kufa na kuchomwa moto yeye na pikipiki yake.

Alisema, Omari aligundulika na wapita njia ambao walitoa taarifa polisi wilaya ya Muheza ambao walifika wakiongozwa na Mkuu wa Upelelezi Wilaya, Charles Ntenga, na kuchukua mwili ambao umehifadhiwa Hospitali Teule ya Muheza.

# Ukaguzi PPRA waibua upigaji bil. 8.77/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UCHUNGUZI na ukaguzi uliofanywa na Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa mwaka wa fedha 2022/23, umebaini serikali imepata hasara ya Sh. bilioni 8.77.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, amesema hiyo ni kutokana na ukosefu wa uwajibikaji, ufanisi, uwazi na uadilifu wa taasisi 12 zilizochunguzwa.

Chande alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupokea ripoti ya tathmini ya utendaji ya mwaka wa fedha 2022/23 kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba.

Alisema vitendo hivyo ni vya jinai vinavyohujumu uchumi wa nchi na ameviagiza vyombo vya kijinai ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuchukua hatua stahiki.

"Ni dhahiri kuwa serikali haitazivumilia hata kidogo taasisi zinazokiuka sheria, kanuni na miongozo ya ununuzi wa umma, hivyo kurudisha nyuma juhudi za kuleta maendeleo zinazofanywa na serikali," alisisitiza Chande.

Alisema serikali itaendelea kuzifanyia kazi changamoto mbalimbali za rasilimali fedha na watu zilizobainishwa ili kuiwezesha mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na ukamilifu.

"Ni matarajio ya serikali kuwa muswada wa sheria uliopitishwa hivi karibuni na Bunge, utatatua kwa kiasi kikubwa changamoto mbalimbali za kisheria zilizobainika," alisema. Chande alisema Rais Samia Suluhu Hassan, ameendelea kuongoza kwa vitendo kwa kuchukua hatua mbalimbali za kuchochea ukuaji wa uchumi husasan sekta ya ununuzi wa umma ambayo huchukua zaidi ya asilimia 70 ya matumizi ya fedha za serikali.

"Kwa mantiki hiyo, limekuwa ni eneo muhimu kutokana na fedha nyingi za serikali kutumika," alisema.

Alisema maelekezo na miongozo ya Rais aliyotoa kuhusu kufanyia maboresho sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zinazosimamia sekta ya ununuzi wa umma, kazi kubwa imefanyika ndani ya kipindi kifupi.

"Hivyo tutarajie manufaa makubwa kwa taifa letu kwa msingi huo, tunamwahidi (Rais) kuendelea kusimamia kwa ukamilifu miongozo na maelekezo yake katika kuboresha sekta ya ununuzi wa umma,"alisema.

Chande aliipongeza Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya PPRA kwa kuendelea kusimamia na kudhibiti michakato ya ununuzi wa umma kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo. "Niwapongeze kwa kutekeleza matakwa ya serikali ya kujenga Mfumo wa Ununuzi wa Kielektroniki wa Taifa (NeST) utakaotumika kuongeza uwazi na kuziba mianya ya rushwa kwenye ununuzi wa umma,"alisema.

Alisema hatua hiyo itawezesha ushiriki sawa wa makundi maalum hususan wanawake katika michakato ya ununuzi wa umma. Pia alisema hatua hiyo itasaidia kudhibiti matumizi mabaya ya ofisi na upotevu wa fedha za umma.

Hata hivyo, alisema katika mwaka wa fedha husika, mamlaka ilifanya ufuatiliaji kuhusu matumizi ya mfumo wa TANePS ambapo matokeo yalibainisha kuwa taasisi 132 kati ya 864 hazikutumia mfumo katika ununuzi wao, kitendo ambacho ni ukiukwaji wa sheria, kanuni na maelekezo ya serikali.

"Ninazikumbusha taasisi nunuzi zote za serikali kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 2 wa mwaka 2023/24 unaozielekeza Taasisi Nunuzi zote kuhakikisha zinafanya ununuzi wa umma kupitia mfumo wa NeST kuanzia Oktoba Mosi, 2023.

"Naagiza hatua kali zichukuliwe kwa wote watakaokiuka maelekezo haya, Katibu Mkuu Hazina na Mlipaji Mkuu wa Serikali ninakuelekeza kuwa, hili ulisimamie na kulifuatilia kwa karibu," alielekeza.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Yanga, Simba msibweteke bado hamjamaliza kazi CAF

**SIMBA** na Yanga zote kutoka Ilala jijini, Dar es Salaam zinatarajia kushuka dimbani nyumbani wikendi hii kwa ajili ya kucheza mechi zao za marudiano za mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga itakuwa ya kwanza kuwakaribisha Al Merrikh leo kuanzia saa 2:00 usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi wakati kesho Wekundu wa Msimbazi watawaalika Wazambia, Power Dynamos kwenye uwanja huo huo.

Mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga watashuka kuwavaa wapinzani wao wakiwa mbele kwa ushindi wa mabao 2-0, ambao waliupata katika mchezo wa kwanza uliochezwa Septemba 16, mwaka huu huko Kigali, Rwanda.

Vigogo wa Sudan, Al Merrikh walitumia Uwanja wa Pele Kigali, ulioko katika eneo la Nyamirambo kwa sababu za kiusalama zilizoko nchini kwao, kwa maana hiyo timu zote zilionekana ziko ugenini huku Simba kesho itawakaribisha Power Dynamo, wenyeji wa Ndola, Zambia.

Hata hivyo, Simba katika mechi hiyo ya kwanza ililazimishwa sare ya mabao 2-2, shukrani kiungo Mzambia, Clatous Chama kwa kufunga mabao yote mawili kwa upande wa kikosi hicho cha Msimbazi.

Singida Fountain Gate FC ya mkoani Singida ni timu nyingine iliyobakia inayopeperusha bendera ya Tanzania katika mashindano ya kimataifa, wawakilishi hawa wanachuana katika michuano ya Kombe la Shirikisho, wao wako ugenini Misri kwa ajili ya kuwakabili Future, mechi yao ya marudiano ikipangwa kufanyika kesho mjini Cairo.

Walima alizeti hao kesho watateremka dimbani wakiwa mbele kwa ushindi wa bao 1-0, walioupata hapa nyumbani kwenye mchezo wa kwanza, mabosi na benchi ya ufundi la timu hiyo wamekaririwa wakisema maandalizi yote muhimu yamekamilika na hawatashuka uwanjani kinyonge. Simba, Yanga na Singida Fountain Gate zote zinahitaji matokeo ya ushindi wa aina yoyote au sare ya bila kufungana ili kujihakikishia kutinga hatua ya makundi ya mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Endapo timu zote tatu zitatinga hatua ya makundi katika michuano hii ya CAF, si tu zitakuwa zimejiwekea heshima, lakini zitakuwa zimeitangaza vyema Tanzania na kujiweka katika nafasi nyingine kubwa ya kutoa wawakilishi wanne katika mashindano ya msimu ujao.

Mafanikio ya wawakilishi hawa waliobakia pia yataendeleza mwanga mweupe ambao umewashwa na Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ambayo imekata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2024), lakini pia Tanzania ikipata nafasi ya kuwa mwenyeji kwa kuandaa AFCON 2027. Katika kuhakikisha timu zote zinasonga mbele, tunazikumbuka kushuka uwanjani kwa ajili ya kupambana na kusahau matokeo ya mechi zilizotangulia, wanatakiwa wafahamu wapinzani wao pia wanaweza kusaka matokeo bora na hivyo watawaondoa katika mashindano hayo, jambo ambalo Watanzania hawataki kulisikia kwa sasa. Yanga ambao ilipata ushindi wa mabao 2-0, inaweza kuona imemaliza kazi, lakini kiuhalisia bado kikosi hicho kina jukumu la kuhakikisha wanapata matokeo bora yanayoyowapeleka hatua ya makundi kibabe au kwa heshima, wakumbuke kama wao walipata ushindi ugenini, basi Al Merrikh pia wanaweza kuupata wakiwa hapa Tanzania.

Tunaikumbusha Simba kutorudia makosa waliyofanya katika mchezo wa kwanza, wanatakiwa kuamini wanaweza kupata ushindi na kuendeleza rekodi yao ya kucheza hatua ya makundi ya michuano hiyo kwa msimu wa tano mfululizo. Lakini si isonge mbele kwa kubahatisha, Mnyama anatakiwa apambane kwa kuonyesha soka safi, kuongeza umakini na hatimaye kufikia malengo.

Vile vile tunapenda kuikumbusha Singida Fountain Gate, katika dunia ya sasa hakuna timu ndogo wala kubwa, umakini, utulivu wa wachezaji, ndio siri pekee ambayo inaweza kuwaweka kwenye rekodi mpya ya kutinga hatua ya makundi kwa mara ya kwanza.

Pia Nipashe inapenda kuwakumbusha mashabiki wa soka wa hapa nyumbani kuungana mkono lakini pia kuacha kufanya vitendo vya hujuma kwa kufahamu sasa klabu zao zinapeperusha bendera ya nchi, umoja na ushirikiano ndio siri ya mafanikio kokote.

Kila la kheri Simba, Yanga na Singida Fountain Gate.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

## Wakati ni huu kuandaa kikosi cha AFCON 2027

**KWA** mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu tangu ijipatie Uhuru kutoka kwa Waingereza mwaka 1961, Tanzania imepata nafasi ya kuandaa Fainali za Kombe Mataifa ya Afrika zitakazofanyika mwaka 2027 (AFCON 2027).

Itakuwa mwenyeji kwa kushirikiana na majirani zake wa Afrika Mashariki, Kenya na Uganda ambazo pia zinaingia katika historia hiyo.

Jumatano iliyopita ilikuwa ni siku isiyosahaulika pale, Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Patrice Motsepe aliponyanyuka na kutangaza rasmi nchi hizo tatu ndiyo mwenyeji wa michuano hiyo mikubwa zaidi Afrika kwa mwaka 2027.

Wakati wa kutangazwa jijini Cairo, Misri ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), Wallace Karia, makamu wake, Athumani Nyamlani na Mkurugenzi wa Sheria, Habari na Masoko wa shirikisho hilo, Boniface Wambura pamoja na maofisa wengine wa serikali.

Mara baada ya kutangazwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan alionyesha kufurahishwa na hilo na akaposti kwenye akaunti yake ya instagram.;

"Pongezi kwa Twiga Stars kwa ushindi katika mchezo wa kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON 2024) kwa kuiondoa Ivory Coast. Nawatakia kila la kheri katika hatua zinazofuata. Kama nilivyoahidi, ushindi huu una zawadi ya motisha. Gerson Msigwa utaratibu ule uendelee." Aliandika Rais Samia.

Rais alionekana kuwa bega kwa bega na mchakato huo wa maombi tangu mwanzo na kusisitiza mara kwa mara kwenye hafla ya michezo, akihimiza miundombinu ifanyike ili ikitokea kukubaliwa maombi basi kusiwe na muda mrefu kabla kukamilika kwa miundombinu, ikiwamo kujenga viwanja vipya, katika majiji ya Arusha na Dodoma.

Katibu mkuu mpya wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa amesema si upande wa michezo tu utakaofaidika na kunufaika na wenyeji wa fainali hizo, bali katika sekta nyingine mbalimbali kama utalii, hoteli, usafirishaji, vyakula na hata nyumba za kupangisha kutokana na kupokea wageni wengi watakaokuja kucheza, kuchezesha, kuangalia, kuripoti, kushabikia timu zao kutoka nchi mbalimbali za Afrika na dunia kwa ujumla.

Tayari ndoto zimetimia, kilichobaki sasa ni kuandaa kikosi imara kitakachoiwakilisha Tanzania katika michuano hiyo.

Kuwa mwenyeji ni moja kwa moja Taifa Stars imetinga fainali hizo, pamoja na wenzao wa Kenya na Uganda, hivyo si jambo jema kutoka mapema au kuwa wasindikizaji katika fainali hizo.

Wakati tukiwaacha viongozi wakishughulika na miundombinu, kazi iliyobaki sasa kwa wadau wengine waliobaki ni kutengeneza wachezaji bora kwa ajili ya fainali hizo.

Kwa hawa wachezaji waliopo sasa na watakaocheza AFCON mwakani huko Ivory Coast, sidhani kama wengi wao watakuwepo kwenye kikosi cha fainali za 2027.

Ni wajibu sasa wadau wa soka wakiwamo makocha kutengeneza wachezaji vijana wa Kitanzania watakaotuwakilisha vyema kwenye michuano hiyo ikiwezekana ifike hatua ya kuanzia robo fainali kama si kuchukua ubingwa kabisa.

Tumefuzu jambo moja la kupata wenyeji na kutinga fainali, lakini sasa tunatakiwa kutengeneza kikosi ambacho kitakuwa cha kushindana na si kusindikiza.

Najua kwa Tanzania kutwaa AFCON moja kwa moja linaweza kuwa jambo gumu, lakini tunachotakiwa tuwe washindani na si wasindikizaji, ili kuwaambia watu lengo halikuwa kuwa mwenyeji tu, bali hata kuwaonyesha watu Tanzania iko juu kwa sasa kisoka kuliko wakati mwingine wowote.

Muda bado upo, kutoka sasa mpaka 2027 si haba, kama tukidhamiria tunaweza kutengeneza hata vikosi viwili vya wachezaji bora kabisa ambao wanaweza kuiwakilisha nchi kwa ubora mkubwa.

Wachezaji hao watapatikana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Championship, First Leaguei na hata wasaka vipaji wanaweza kusaidia kupatikana kwao ili kuipa Taifa Stars iliyo bora na imara itakayokuwa ikicheza mbele ya maelfu ya mashabiki wake nchini na kuwapa furaha.

MAKALA MAALUM

DK. SALIM AHMED SALIM...

# Yajue makubwa yake kibalozi hadi tuzo alizotwaa kimataifa

Na Peter Orwa

**JUMATANO wiki hii ilikuwa sehemu ya pili ya simulizi ya maisha ya mwanadiplomasia Dk. Salim Ahmed Salim, ikiendeleza wasifu na chimbuko lake, ufafanuzi ulioanza Jumatano wiki iliyopita. Leo akiwa anazindua tovuti inayomhusu. Pata sehemu ya mwisho ya ufafanuzi;**



LEO kuna tovuti maalum inazinduliwa, ikihusu wasifu wa mwanadiplomasia wa Afrika, Mtanzania Dk. Salim Ahmed Salim (pichani), ukiwa ni mwendelezo wa historia yake inayozidi kung'arishwa, akitimu umri wa miaka 81 sasa.

Ni miaka 59 iliyopita, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikihesabu miezi tu mwaka 1964, ikaweka rekodi ya kupata balozi kijana akiwa na umri wa miaka 59, wakati huo yu mwenye umri miaka 22.

Naye hakumuangusha aliyemteua, Rais wake Julius Nyerere, pale alipoweka rekodi iliyotukuka kiutendaji, ikiwamo bado kidogo kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, mwaka 1981.

Bado akaonyesha makali yake kidiploamsia, akiwa Rais wa Bunge la Ulaya na Balozi wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa.

Dk. Salim alianza kuwa Balozi nchini Misri, wakati huo akinena mwenyewe utashi wake zaidi ulikuwa kubaki Zanzibar, kutumikia maendeleo ya nchi changa ya nyumbani.

Hadi kufika mwaka 1965, Dk. Salim akiwa balozi nchini India, ambako alitumia vyema uzoefu wake wa Zanzibar kuendeleza siasa zake ughaibuni akiwa mwakilishi maalum, damu yake ikiwa changa.

Utashi na upevu wake katika uongozi ulimgusa zaidi Rais Nyerere, hasa pale walipokutana naye katika kikao cha Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU), jijini Cairo Misri, hasa wanapochangia kwa pamoja fikra kuelezea Azimio la Arusha, utaifishaji wa mali wakijenga jamii mpya ya kijamaa na dhana ya Ujamaa na Kujitegemea.

Baadaye katika utumishi wake huo, akawa balozi nchini China, taifa ambalo katika harakati zake za ukombozi wa Zanzibar, amewahi kukutana na Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Chuo En Lai, katika enzi zake muda mfupi kabla ya uhuru, wakati huo akiwa mwanahabari.

Ni katika hilo, akasifika hata akiwa nchini China anabaki katika rekodi ya umahiri kuboresha diplomasia ya Tanzania na China, wakati huo urafiki unaimarishwa hasa, chini ya Waziri Mkuu Chuo Enlai na Rais Mao Tse Tung.

Hata pale alipokuwa Misri, nchi hiyo chini ya utawala wa Rais Gamal Abdel Nasser, akiwa na sera zilizofanana na sera ya Tanzania katika kuunga mkono ukombozi wa Tanzania, wakizipa silaha nchi hizo kufanikisha azma, juhdi zake balozi huyo zikashuhudiwa akiwa kiunganishi wa nchi.

Pia, ameshakuwa Rais wa Bunge la Umoja wa mataifa, kati ya Mwaka 1979 na 1980.

Ni kwa kiasi kikubwa nyendo nyingi za ukombozi zilichukua katika nafasi, mwanzo wake katika ofisi za Cairo na Dar es Salaam. Salim Ahmed Salim, mzaliwa wa Januari 23, mwaka 1942, akiwa tena katika jukumu la kisiasa aliloacha mwaka 1964 nyumbani na kuingia katika diplomasia.

Akarudia siasa mwaka 1981 akiwa waziri na kwamba ilipofika Aprili 24, mwaka 1984 hadi Novemba 1985 akawa Waziri Mkuu wa tano nchini. Mwaka 1989, akawa Katibu Mkuu wa Umoja wa Nchi Huru Afrika - OAU (sumulizi ya wiki iliyopita) akiwa mzizi wa kuhamia Umoja wa Afrika AU na baadhi ya sera sasa.

**TUZO ZA TAALUMA**

Ana shahada nyingi ngazi ya uzamivu, katunukiwa zikiwamo nchini Sudan, katika Masuala ya Kimataifa (1995); nyingine ni Chuo Kikuu cha Bologna, Italia (1996) katika Uhusiano wa Kimataifa; Chuo Kikuu cha Cape Town Afrika Kusini (1998) na Chuo Kikuu cha Addis Ababa, Ethiopia (2003), zote katika sheria.

Vilevile, Dk Salim ana tuzo na nishani nyingi. Kapata tuzo katika nchi za Liberia (1980), Tanzania (1985), Nishani ya Kitaifa ya Vilima Elfu Moja, Rwanda (1993), Jamhuri ya Congo, Nishani ya Kipendo (Msalaba Tukufu) - 1994, Nishani ya Sifa (Ofisa Tukufu) ya Jamhuri ya Afrika ya Kati (1994), Medali ya Afrika (1999), Senegal, Nishani ya Kitaifa cha Simba (Ofisa Tukufu) - 2000; Nishani ya Mito Miwili Naili Sudan (2001); Nishani ya El-Athir, Algeria 2001.

Pia kuna; Nishani ya Mono, Togo (2001); Nishani ya Kitaifa cha Mali (Kamanda) Mali, 2001; Nishani ya Masahaba wa O.R.Tambo, Afrika Kusini (2004); Nishani ya Mwenge Daraja la Pili (2011), Tanzania.

# Viwanda 200 kuonyesha bidhaa Dar

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade), imeandaa maonyesho makubwa ya kimataifa ya viwanda.

Katika maonyesho hayo ya Tanzania International Manufactures TIMEXPO 2023, zaidi ya viwanda 200 vya ndani na nje ya nchi vinatarajia kushiriki.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa CTI, Leodegar Tenga, alisema mgeni rasmi katika ufunguzi wa maonyesho hayo yatakayofanyika katika ukumbi wa Diamond Jubilee kwa siku tatu kuanzia Oktoba nne, anatarajiwa kuwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Tenga aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki maonyesho hayo ili kujionea teknolojia mpya na bidhaa mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

"Maonyesho kama haya ambapo wenye viwanda pekee wanakuja kuonyesha teknolojia mpya mbalimbali wanazotumia kwenye uzalishaji wa bidhaa zao ni mara chache sana kutokea hapa nchini, ndiyo maana CTI na Tantrade tunayachukulia maonyesho haya kwa umuhimu mkubwa.

"Viwanda vyote vikubwa hapa nchini vimo na wahusika wameshajiandikisha, tunawaomba wote washiriki kwa sababu hili ni jambo lao, waje kuonyesha nini wanafanya ili tuweze kutangaza sekta hii ya uzalishaji viwandani ambayo tunaona ndiyo mhimili wa uchumi wetu," alisema Tenga. Alisema katika maonyesho hayo, viwanda vikubwa duniani vikiwamo vile vinavyotengeneza ndege vitashiriki na vitaonyesha namna zinavyotengenezwa kuanzia hatua ya awali kabisa mpaka kupaa angani.

Mkurugenzi wa Uhamasishaji Biashara wa TanTrade, Fortunatus Mhambe, alisema maonyesho hayo ni makubwa ya aina yake kuwahi kutoka nchini, hivyo aliwataka Watanzania washiriki kikamilifu.

Alisema TanTrade imekuwa ikiandaa maonyesho ya viwanda mara kadhaa, lakini mwaka huu imeona ije na picha nyingine tofauti kuonyesha bidhaa za viwandani pekee kama hatua ya kuimarisha uhusiano wa sekta binafsi na sekta ya umma.

"Kwetu haya ni mafanikio makubwa sana kwa sababu tumeona viwanda mbalimbali vitakavyoshiriki kwa upande wa kilimo, teknolojia, ujenzi, kemikali za viwandani, wote hawa wamesema watashiriki kuonyesha huduma zao kwa hiyo, tunapenda kuendelea kuwahamasisha waendelee kujiandikisha washiriki maonyesho," alisema Mhambe.

Alisema maonyesho hayo yatakuwa fursa kubwa kwa wenye viwanda kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili kwani viongozi wa taasisi mbalimbali za serikali wakiwamo mawaziri watashiriki.

"Haya hayatakuwa maonyesho tu, bali fursa muhimu kwa wenye viwanda kuelezea changamoto zao na kupata majibu ya hapo hapo. Wananchi nao waje waone ubunifu na teknolojia mbalimbali za kisasa zitakazokuwapo pale. Hii ni fursa ambayo siyo ya kukosa, na kutakuwa na kiwanda cha kutengeneza ndege kitaonyesha kinavyotengeneza kuanzia mwanzo," alisisitiza.



Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke (kushoto), akiwa na wadau wengine wa benki hiyo, akiwemo Mkurugenzi wa Fedha wa Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania (TMRC), Oswald Urassa (kulia), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Ujenzi ya CPS, Sebastian Dietzold (wa pili kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Nabaki Afrika, Russel Stuart (pili kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Mkakati cha benki hiyo, Msafiri Shayo wakifuatilia mada mbalimbali zilizokuwa zinawasilishwa wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Mkopo wa Nyumba wa NBC, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Benki imetangaza uzinduzi mtandao

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imetangaza uzinduzi wa mtandao wake wa mazungumzo ya benki unaoitwa Kai, uliokusudiwa kubadilisha sekta ya benki.

Mkuu wa Biashara wa benki hiyo, Fredrick Max, alisema jana kuwa hatua hiyo ya kipekee inathibitisha dhamira thabiti ya benki katika kutoa suluhisho za ubunifu na kuboresha kuridhika kwa wateja.

Alikuwa akizungumza wakati wa warsha iliyojadili maendeleo yaliyopatikana katika nafasi ya kidijitali, iliyofanyika mwishoni mwa wiki.

Alisema Kai, mtandao wa mazungumzo rafiki na wenye ufanisi, inachukua enzi mpya jinsi watumiaji wanavyopata taarifa za benki na msaada na itaharakisha na kufanya huduma na bidhaa za benki kuwa za kufikika zaidi.

"Tunafurahi kuanzisha Kai, hatua kubwa mbele katika uboreshaji wetu wa kidijitali na Kai inaongeza kasi ambayo tutahudumia wateja wetu, ikiwa ni pamoja na biashara ndogo na za kati na inaonyesha dhamira yetu ya kukidhi mahitaji yanayobadilika ya wateja wetu wanaothaminiwa kwa kutoa uzoefu wa benki ambao si tu wa kufikika zaidi bali pia ni wa ufanisi zaidi," alisema.

Alisema Kai inalingana kabisa na malengo ya biashara na wateja ya Stanbic kwa kuwa inawakilisha hatua mkakati kuelekea ufanisi na ufikika mkubwa zaidi katika huduma zake.

Pia, alisema ubunifu huo si tu unaboresha michakato ndani ya benki lakini pia unathibitisha tena dhamira ya benki kuwa mstari wa mbele katika teknolojia ya benki. "Kwa wateja wetu wanaothaminiwa, Kai inawakilisha hatua kubwa katika kuboresha uzoefu wao wa benki. Tumejitolea kuwapa zana na msaada wanahitaji kusafiri katika safari zao za kifedha kwa urahisi. Uzinduzi wa Kai unaturuhusu kuwahudumia vyema mahitaji yao yanayobadilika, kutoa njia ya haraka na ya rahisi zaidi ya kushiriki na akaunti zao na shughuli zao," aliongeza Max.

# Tovuti ya hifadhi nyaraka Dk. Salim kuzinduliwa leo

**Na Mwandishi Wetu**

TOVUTI ya hifadhi ya nyaraka za Dk. Salim Ahmed Salim, mwanadiplomasia mashuhuri nchini, inatarajiwa kuzinduliwa kesho, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Dk. Salim aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Katibu Mkuu wa nane wa Jumuiya ya Muungano wa Nchi za Afrika (OAU) kuanzia mwaka 1989 – 2001, tovuti yake inatarajiwa kuzinduliwa Septemba 30. Taarifa iliyotolewa na familia ya Dk. Salim, ilisema mgeni rasmi katika tukio hilo ni Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. Pia, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi atashiriki katika uzinduzi huo.

Wageni wengine ni pamoja na viongozi waandamizi kutoka kwenye sekta za umma na binafsi; viongozi wastaafu; na wawakilishi wa washirika wa maendeleo, asasi za kiraia, na taasisi za elimu ya juu.

Taarifa hiyo ilisema tovuti hiyo; www.salimahmedsalim.com inajumuisha video, picha na nyaraka mbalimbali (zikiwamo hotuba, nakala za mawasiliano ya kimaandishi, na machapisho ya kitafiti) za Dk. Salim. Pia, inatoa ujuzi wa kipekee kuhusu safari yake ya utumishi wa umma, na mchango wake katika mahusiano ya kimataifa na jitihada za ukombozi barani Afrika. Aidha, inaangazia mchango wa nchi za Afrika katika siasa za kimataifa katika kipindi cha mwaka 1960 hadi 2000. Tovuti hiyo imeandaliwa na familia ya Dk. Salim kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na ndugu, jamaa na marafiki.

Aidha, tovuti hiyo ambayo ni hifadhi ya matukio yaliyotengeneza maisha ya Dk. Salim, na muhimu zaidi, hifadhi ya nukuu na nyaraka zake mwenyewe, inalenga kuimarisha historia ya Tanzania na ile ya Afrika. Nyaraka za tovuti hii zitawavutia wale wanaotaka kuelewa mchango wa Tanzania na wa nchi nyingine barani Afrika katika historia ya dunia na siasa za kimataifa.



## HABARI DODOMA

# 59,000 hufa kwa kichaa cha mbwa kila mwaka

**Na Paul Mabeja**, MPWAPWA

WATU 59,000 wanapoteza maisha kila mwaka duniani kutokana na ugonjwa wa kichaa cha mbwa na asilimia 36 ya vifo hivyo hutokea katika bara la Afrika.

Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Arbogast Warioba, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza kwenye Maadhimisho ya Siku ya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa Duniani iliyofanyika kitaifa wilayani hapa.

"Asilimia 30 hadi 50 ya waathirika wa ugonjwa huu ni watoto chini ya miaka 15 kwa sababu ndio wamekuwa karibu na mbwa wanaofugwa kwa muda mwingi, pia hupenda kuchokoza mbwa wasiomfahamu njiani na kusababisha kung'atwa," alisema.

Aidha, alisema katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Agosti, mwaka huu, watu 20,005 nchini walitolewa taarifa ya kung'atwa na wanyama.

"Zaidi ya watu 20,000 wameripotiwa kung'atwa na mbwa kwa kipindi cha Januari hadi Agosti mwaka huu ambapo Mkoa wa Dar es Salaam unaongoza ukifuatiwa na mikoa ya Dodoma, Morogoro na Arusha," alisema.

Alisema Dar es Salaam inaongoza kwa kuwa na matukio 3,321, Dodoma 3,136, Morogoro 1,559 na Arusha 1,155 na kwamba takwimu hizo zinajumuisha wananchi waliopata huduma za matibabu katika vituo vya afya.

"Vimelea vya ugonjwa wa kichaa cha mbwa vinapoingia katika jeraha hushambulia mfumo wa fahamu kuanzia katika eneo la jeraha, kuelekea uti wa mgongo na hatimaye kuathiri mfumo wa kati ya fahamu (ubongo)," alisema.

Alisema ili kudhibiti ugonjwa huo, serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma, kuboresha utekelezaji wa afya nchini, kurahisisha upatikanaji wa huduma za chanjo ya kichaa cha mbwa kwa wananchi na kurahisisha upatikanaji wa huduma ya chanjo kwa wanyama hasa mbwa na paka.

"Serikali imeshiriki katika michakato ya kidunia ambayo imewezesha mwaka huu Shirika la Usambazaji Chanjo Duniani (GAVI) kuridhia chanjo ya kuzuia kichaa cha mbwa kuingizwa katika mfumo wa chanjo za kawaida. "Gharama zinatarajiwa kushuka zaidi pale taratibu za utekelezaji wa jambo hilo utakapokamilika," alisema.

Dk. Robert Kishimba kutoka Wizara ya Afya, alisema pamoja na juhudi za kutokomeza, ugonjwa huo bado ni janga na hivyo ni lazima kuepuka kwa kuwakinga wanyama kama mbwa, paka na wengine.

Alisema jamii inapaswa kuepuka tabia hatarishi za kuwachokoza na kuwapiga mbwa ikiwa ni pamoja na kuelimisha watoto wasicheze na mbwa wasiyemfahamu.

# Upasuaji ubongo kwa matundu mbioni kufanyika nchini

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

MADAKTARI bingwa wa upasuaji wa mifumo ya fahamu, ubongo na uti wa mgongo nchini wanatarajia kupewa mafunzo ya wa kutoa huduma kwa wagonjwa bila ya kufungua fuvu.

Mafunzo hayo yatakayoanza Oktoba mosi hadi sita na kuongozwa na madaktari bingwa kutoka nchini Japan, ni hatua za awali za kuanza utoaji huduma hiyo katika hospitali kubwa nchini.

Mafunzo hayo ambayo yatawashikisha pia madaktari bingwa wa nchini yanatarajia kufanyika katika Hospitali ya Kanda ya Rufaa ya Benjamin Mkapa (BMH) jijini Dodoma.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mifumo ya Fahamu, Uti wa Mgongo na Ubongo wa BMH, Henry Humba alisema kuwa upasuaji huo kwa njia ya matundu unapunguza gharama za matibabu, muda wa mgonjwa kuuguza jeraha na wa daktari kufanya upasuaji.

Kwa mujibu wa Dk. Humba, mafunzo hayo yatahudhuriwa na madaktari kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa, Mnazi Mmoja Zanzibar, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Mloganzila, Bugando, KCMC, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na Agha Khan.

Alifafanua kuwa mafunzo hayo ni hatua za awali za Hospitali ya Benjamin Mkapa kuanza kutoa huduma za upasuaji huo bila kufungua fuvu ili kukuza utalii wa matibabu nchini.

"Serikali ilikwisha leta vifaa ikiwemo mashine ya kuwezesha kufanyika kwa upasuaji huu, kwa hiyo mafunzo haya ni hatua muhimu sana kwetu tunapoelekea kutumia mbinu hizo kutoa huduma," alisisitiza Humba.

Alisema Profesa Akio Hyodo, bingwa mbobezi na mshauri wa huduma za upasuaji huo , ataongoza jopo la wataalamu wenzake wanne kutoka Japan kuendesha mafunzo hayo.

"Tutaanza kwa mjadala wa kitaaluma kutathimini hali halisi ya utoaji wa huduma za upasuaji wa mifumo ya fahamu, uti wa mgongo na ubongo nchini kulekea kwenye ujuzi wa juu wa utoaji wa huduma hizo," alisema.

Alisema ujio wa Profesa Hyodo na ujumbe wake ni maandalizi ya BMH kupokea mashine nyingine mpya ya kisasa itakayoimarisha utoaji wa huduma za upasuaji huo.

Alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa ahadi iliyotolewa na Dk. Higashiue Shinichi, Mwenyekiti wa Tokushukai Medical Corporation ambao ni wadau muhimu wa Hospitali ya Benjamin Mkapa.




Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu akizungumza na wakuu wa mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), kutoka mikoa na wakuu wa upelelezi (hawapo pichani), jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Halmashauri yakopesha vijana, wanawake, walemavu mamilioni

**Na Thobias Mwanakatwe**, MANYONI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida imetoa mikopo ya Sh.milioni 108 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wilayani hapa hadi kufikia Juni mwaka huu kwa ajili ya kuanzisha miradi ya ujasiriamali na kuondokana na umasikini.

Hayo yamo katika risala ya Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Kemirembe Lwota ya utii kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan aliyoisoma juzi wakati wa kuhitimisha mbio za Mwenge wa Uhuru wilayani hapa.

Lwota alisema kuwa mikopo hiyo ambayo ni sawa na asilimia 48 ni kati ya Sh.milioni 224.4 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa makundi hayo katika mwaka wa fedha 2022/23.

Alisema Mwenge wa Uhuru ukiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni umetembelea na kukagua miradi yenye thamani ya Sh.bilioni 1.236.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni ujenzi wa barabara ya Manyoni-Msigati yenye urefu wa mita 700 kwa kiwango cha lami nyepesi kwa gharama ya Sh.milioni 589.

Mradi wa uhifadhi wa chanzo cha maji Kaloleni unaohudumia wakazi 5,271 wa mitaa ya Ujasiriamali, Mwanzi, Mitoo ya Chini, Kaloleni na Samaria.

Mwingine ni ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho katika Kijiji cha Ilucha kwa Sh.milioni 568, Zahanati ya Kijiji cha Mbwasa kwa Sh. milioni 77.6 ambayo itahuhudumia wakazi 2,526.

Miradi mingine iliyotembelewa na Mwenge huo ni ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ya elimu ya awali katika Kijiji cha Chikuyu kwa Sh.milioni 64.9, kikundi cha vijana cha Imani - Majiru ambao wamenunua bajaj na mradi wa madawati 300 yaliyonunuliwa kwa Halmashuri ya Wilya ya Manyoni kwa Sh.milioni 21.

Kiongozi wa mbio hizo Kitaifa kwa mwaka huu, Abdalla Shaibu Kaim, akizungumza baada ya kutembelea mradi wa maji Kaloleni, aliwataka wananchi kulinda vyanzo vya maji kwa kutofanya shughuli za kilimo na ufugaji.

Kaimu alisisitiza kuwa sheria ipo wazi kuwa hairuhusiwi kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya vyanzo vya maji mita 60 na kuwaagiza viongozi wa wilaya hiyo kuimarisha ulinzi ili visiharibiwe.



## Zanzibar yaongezewa mgawo wa fedha za misaada

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema changamoto za Muungano zinaendelea kupatiwa ufumbuzi hatua kwa hatua ikiwemo mgao wa Zanzibar katika fedha za misaada ya kibajeti kuongezwa hadi kufikia asilimia tisa.

Hayo yalisemwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dk.Sada Mkuya Salum wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Wingwi, Kombo Mwinyi Shehe aliyetaka kujua kwa kiasi gani changamoto za kero za Muungano zinafanyiwa kazi katika sekta ya uchumi na fedha.

Dk. Salum alisema mgao kwa Zanzibar unaotokana na misaada ya fedha za kibajeti GBS kutoka asilimia 4.5 hadi kufikia asilimia 9 na ni matokeo ya mashauriano ya Wizara ya Fedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na wizara yake katika kuona changamoto za kifedha na kiuchumi zinafanyiwa kazi.

Alisema mashauri hayo yanatokana na uchambuzi wa kina wa kitaalamu juu ya masuala ya uchumi, sera za fedha, utawala na idadi ya watu.

Dk Mkuya alisema mazungumzo hayo yamechukua muda mrefu kwa pande hizo na kutafuta mshauri mwelekezi wa kufanya kazi za uchambuzi kupitia fedha za misaada zinazopatiwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na mgawanyo wake.

"Mheshimiwa Spika napenda kuchukua nafasi hii kutoa salamu zangu za shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kulipatia ufumbuzi tatizo hili la muda mrefu kuhusu mgao wa Zanzibar katika fedha za lengo lake ni kuzipatia ufumbuzi changamoto zote za Muungano katika masuala ya kifedha na uchumi wa kibajeti, " alisema.

Waziri huyo alisema kwa mujibu wa makubaliano ya pande hizo utekelezaji wa gawio jipya ulitarajiwa kuanza Julai mwaka huu, hadi sasa hakuna mgao uliofanyika. Alizitaja sababu hizo ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Muungano bado haijapokea fedha za kibajeti zinazotokana na msaada kutoka kwa washiriki wa maendeleo.

"Mheshimiwa Spika niseme kwa ufupi kwamba hadi sasa bado Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijapokea fedha zinazotokana na mgao wa kibajeti kutoka kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambazo hutokana na washiriki wa maendeleo, " alisema.

# Wafanyabiashara: Ushushaji mizigo umezorota Malindi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAFANYABIASHA wa Bandari ya Malindi visiwani Zanzibar, wamesema bado kuna uzorotaji na ucheleweshaji ushushaji na upakiaji wa mizigo katika bandari hiyo licha ya kubinafsishwa kwa Kampuni ya Africa Global Logistics (AGL) ya Ufaransa.

Wakizungumza na Nipashe, wafanyabiashara hao walisema bado ufanisi wa kazi haupo vizuri hali ambayo imepelekea kwa muda wa wiki moja sasa wameshindwa kushusha mizigo yao.

"Ufanisi wa kazi bado wanachelewa kushusha mizigo lakini ina masharti yao ni makubwa waliyoweka bandarini hapo," alisema Ali Yahya, mtoaji, muingizaji na msafirishaji wa mizigo.

Alisema ni vema kampuni hiyo wapunguze masharti kwa sababu bandari hiyo ni ndogo haina nafasi ya kuhifadhi makontena mengi.

"Moja ya masharti yao kama kontena zikipangwa chini, kontena ya pili usikate mzigo, lazima tutumie akili bandari yetu ni ndogo walikuwa wasiweke masharti kwanza kwa sababu kunapelekea mfumuko wa bei wa bidhaa kwa sababu bidhaa zinachelewa kutolewa," alisema.

Alisema kabla ya kuweka masharti yao, ilipaswa kwanza watoe elimu kwa wafanyabiashara na washushaji wa mizigo bandarini hapo kwa sababu wengi wa wachukuzi wa mizigo hawana kiwango kikubwa cha elimu, hivyo wanahitaji kuelekezwa.

Aliitaja changamoto nyingine kuwa ni ucheleweshaji wa upatikanaji wa stakabadhi za mizigo na mzunguko mkubwa kulipia ushuru.

"Kampuni imekuja lakini lazima watu wa bandari kutoa ushirikiano ili kutowaumiza wafanyabiashara, bandari ikifika saa 9:30 alasiri inafungwa hakuna kutoa mizigo umeona wapi bandari haifanyi kazi kama shule," alisema.

Alisema walitarajia kampuni hiyo itarahisisiha maendeleo bandarini hapo badala yake kumekuwa na ucheleweshaji wa upatikanaji wa mizigo.

Katika kupunguza msongamano wa makontena ya mizigo katika bandari hiyo, kampuni inayosimamia uendeshaji wa Bandari, Zanzibar Multipurpose Terminal (ZMT) kupitia AGL imesema inatarajia kujenga bohari ya makontena nje ya bandari hiyo.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Mkurugenzi Mtendaji wa ZMT, Nicolas Escalin, alisema lengo ni kuboresha uzalishaji wa bandari na ufanisi kwa manufaa ya wananchi na uchumi wa Zanzibar.

Alisema katika kusimamia vifaa vya bandari, ZMT inalenga kujenga miundombinu ya kisasa yenye uwezo ili kuhakikisha mtiririko mzuri wa uagizaji mizigo na mauzo ya nje ya nchi, kulingana na viwango vya kimataifa. Alisema tangu AGL ikabidhiwe na serikali, kampuni yake imeanza kufanya kazi ya kushusha makontena 300 ya mizigo lengo ikiwa ni kuhudumia mahitaji ya uagizaji na usafirishaji wa kanda.

Alisema kampuni hiyo pia imechukua wafanyakazi 400 wa Shirika la Bandari ya Zanzibar, ambao walikuwa wakifanya kazi Bandari ya Malindi.


Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari Zanzibar, Nahaat Mahfoud, alisema ushirikiano huo unaimarika kwa lengo la kuwa na kituo kikuu cha usafirishaji katika kanda.

Alisema kuwa bandari mpya inayoendeshwa na AGL, ni ya kwanza ya aina yake Afrika Mashariki na ni harakati zake za kupanua huduma barani Afrika.

Akizungumzia kuhusu ZMT alisema ni waendeshaji wa kituo cha Malindi kilichopo Zanzibar na wanahisa wake wa kumbukumbu AGL.

Alisema AGL ni mhusika mkuu katika usafirishaji Afrika na SEGA, mshirika wake wa ndani, wanalenga kuifanya Bandari ya Malindi kuwa kigezo Afrika Mashariki.

Alisema, mpango wa uwekezaji unatekelezwa ili kuipatia Zanzibar miundombinu ya kisasa, kulinda na kuendeleza ajira na ujuzi wa wafanyakazi na ni moja ya mikakati na vipaumbele vya maendeleo.



Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Othman ataka sera ya mazingira inufanishe wananchi Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amezitaka mamlaka kuhakikisha mapitio ya Sera ya Mazingira ya mwaka huu yananufaisha wananchi kwa kuwa wanategemea maliasili zilizopo kwenye maeneo yao.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mchakato wa mapitio ya sera hiyo, alisema visiwa hivyo vinashuhudia mabadiliko makubwa ya kiuchumi na ya kijamii yanayopelekea matumizi makubwa ya maliasili zilizopo.

Alisema matumizi hayo yanachangia kwa kiasi kikubwa, kuongeza shinikizo katika ikolojia za baharini na nchi kavu.

Alisema kinachodhihirisha ni kuwa mabadiliko ya sera hiyo ya mazingira yanahitajika ili kukabiliana na changamoto za kimazingira na kuielekeza nchi katika maendeleo endelevu, matumizi bora ya maliasili zilizopo nchi kavu na baharini.

"Kwa ajili ya kufikia kwenye azma hiyo, ni vyema mchakato wetu wa kupata sera mpya ya mazingira uwe shirikishi katika ngazi zote ili pia kupata maoni kamili ya wadau juu ya mambo muhimu na ya msingi, ambayo yanafaa kuzingatiwa na kuelewa ni upi wajibu wa wadau kuhakikisha utekelezaji wake," alisema.

Othman alisema miaka 10 imepita tangu kuzinduliwa kwa sera hiyo , lakini kumekuwepo na maamuzi ya kitaifa, kikanda na kimataifa yanayoelekeza Visiwa vya Zanzibar kufikia lengo la maendeleo endelevu.

Aliyataja maendeleo hayo ni pamoja na dira ya maendeleo ya Zanzibar ya 2050, mpango wa maendeleo wa Zanzibar wa 2021-2026, mpango wa kuirithisha Zanzibar ya kijani, kusimamia utekelezaji wa mikataba, maazimio na makubaliano ya kimataifa juu ya usimamizi wa mazingira.

"Kama mnavyofahamu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira inalo jukumu kubwa la kuhakikisha nyenzo za usimamizi wa mazingira ambazo ni pamoja na sera, sheria, kanuni, mikakati na miongozo ya kimazingira, zinakuwepo na kutekelezwa kikamilifu ili kusaidia usimamizi bora na endelevu wa mazingira hapa visiwani," alisema.

Alisema Zanzibar katika hali yake ya asili ilikuwa na mazingira mazuri, yenye fukwe za kupendeza, bahari iliyosheheni rasilimali za aina tofauti, udongo wenye rutuba, miti na wanyama, lakini hali hiyo imeanza kubadilika na kuleta changamoto za kimazingira na kuwa tishio kwa maendeleo ya Taifa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, ameshukuru juhudi zinazochukuliwa na serikali kwa kushirikiana na taasisi kupambana na athari za mazingira zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema lengo la mkutano huo ni kupata sera mpya ya mazingira kwa maendeleo endelevu ya Zanzibar.

Mkurugenzi Mtendaji wa Climate Action Network (CAN) Tanzania, Dk. Sixbert Mwanga, alisema taasisi yake inafanyakazi kwa kutarajia mabadiliko endelevu katika ngazi zote.

Dk. Mwanga alisema kupitia nadharia ya 'Think' inalenga katika sera, ubunifu na miongozo ya kisekta sambamba na 'Tank' inayoangaza dhamira ya utekelezaji wa vitendo kwa nyanja zote za maisha ya watu ndani ya jamii.



# ZIIKI YAZIDI KUWAKANA

KAMPUNI ya kimataifa ya Ziiki ambayo inasimamia mapato na kusambaza muziki kwa kidijitali, imeendelea kusisitiza kwamba haihusiki na malalamiko ya baadhi ya wanamuziki ambao wanadai hawajalipwa malipo yao.

Meneja wa kampuni hiyo kwa ukanda wa Afrika mashariki na kati, Camilla Owora amesema wasanii wote walioingia mikataba ya kuwasimamia kazi zao, wanalipwa mapato yao kama inavyotakiwa na kwa wakati kulingana na mtiririko wa ununuzi wa kazi zao katika majukwaa ya muziki.

Hivi karibuni mwanamuziki nyota wa Bongo Fleva, Harmonize alilalamika kuhusu malipo yake pamoja na msanii wake Ibrah, akisema bado hawajalipwa.

Camilla amesema kuwa wao kama kampuni inawasilisha fumu za malipo kwa kila msanii ambaye ana haki ya kulipwa, ila kuna baadhi wanakataa kusaini bila kutoa sababu za msingi.

"Ukusanyaji wa mapato na ulipaji wetu uko wazi, hatuwezi kwenda kinyume na mikataba tuliotiliana saini nao, hata kwa upande wa Harmonize tumempatia fomu kwa ajili ya kulipwa lakini hajatujibu, lakini pesa zake zipo," amesema Camilla.

Akizungumzia majukumu ya kampuni hiyo.

Aidha amekanusha kwamba kampuni hiyo ina hisa za mwanamuziki Diamond Platnumz, akisema msanii huyo ni mteja wao kama ilivyo kwa wasanii mbalimbali duniani kote.

"Diamond Plutnumz hana hisa kwenye kampuni ya Ziiki, tumeingia naye mkataba kwa ajili ya kumsimamia kazi zake kama ilivyo kwa wasanii wa Hapa Tanzania, Kenya, Uganda na DRC," amesisitiza Camilla.

Akizungumzia majukumu ya kampuni hiyo, Meneja huyo ameeleza kuwa kuna aina mbalimbali ya mikataba wanayoingia nao wasanii ikiwamo kusimamia mapato, uratibu na kusaidia usambazaji wa kazi zao.

BASI SAWA

## Ziara wanamuziki Nigeria zashika kasi



ZIARA za wanamuziki wa Nigeria wanaokuja nchini kutoa burudani zinazidi kushika kasi, sasa ni zamu ya mwimbaji Eltee Skhillz, ambaye amekuja kuwapagawisha mashabiki.

Mkali huyo wa muziki atatumbuiza jijini Dar es Salaam Oktoba 1 katika fukwe ya Kidimbwi Beach iliyopo Mbezi.

Msanii huyo anatambulika kwa nyimbo zake kali ikiwamo 'Odg' ambayo kupitia mtandao wa Youtube imetazamwa na watu milioni 4.

## Yartti TM ajichanganya Bongo Fleva

SIKU moja baada ya kuachia wimbo wake mpya, Mood, msanii wa muziki kutoka Ghana Yartti TM, ameweka wazi kuwa ndoto yake kubwa ni kufanya kolabo na wanamuziki wa Bongo Fleva.

Akizungumza na BT jana, Yartti TM, amesema licha ya kufanya vizuri jijini Accra, mipango yake ni kufanikiwa kupenya kwenye soko la Bongo Fleva na kushindana na mastaa wa muziki huo.

"Nimeachia ngoma yangu mpya inaitwa Mood, natamani TV kubwa za Tanzania na Afrika Mashariki zinipe sapoti kwa sababu mimi ni shabiki wa muziki wao pia. Ninaona wazi kuwa nina nafasi yangu kwenye Bongo Fleva," amesema Yartti.





## RAMADHANI BROTHERS WASHUKURU WATANZANIA

WATANZANIA wanaounda kundi la sarakasi la Ramadhani Brothers wamewashukuru mashabiki wao kwa kuwaunga mkono katika shindano la vipaji duniani la America Go Talent na kufanikiwa kushika nafasi ya tano.

Ibrahim Mwaimisye na Fadhili Ramadhani wanaounda kundi hilo wamesema kuingia katika hatua ya fainali sio jambo rahisi, lakini kutokana na watanzania wengi kuwaunga mkono walipata ujasiri wa kufanya kazi katika ubora.

"Tunawashukuru Watanzania kutuunga mkono na kutupa moyo wakati wote tukishiriki shindano la America Go Talent na hatimaye kushika nafasi tano za juu ni jambo la kufurahisha," amesema Fadhili.



## Phina afurahia Sponser

KIBAO kipya cha Mwanamuziki wa Bongo Fleva, Phina kimeelezwa ndio wimbo bora wa Amapiano kwa wasanii wa kike nchini.

Wimbo huo ambao unaitwa 'Sponser' umetambulishwa siku tatu zilizopita umefanikiwa kufanya vyema katika mitandao ya kijamii.

Hata video ya wimbo huo imekuwa bora na inamvutia mtazamaji, huku ikinakshiwa na vituko vya Phina ambavyo vinafananishwa na msanii Vanessa Mdee.

FILAMU

## Mapenzi ni Sumu: Mume wa mwenzio usimpakie wanja

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wa uhai wake, mwanamuziki Dk. Remmy Ongala alishawahi kuimba wimbo mmoja maarufu ulioitwa 'Natoa Onyo.'

Katika wimbo huo, pamoja na mambo mengine aliwaonya wanawake kukaa mbali na waume za watu.

Anasema huwezi kujua wametokea wapi, huenda walilala chini, walilala na njaa mpaka kufika hapo, leo hii wana maisha mazuri, anatokea sistaduu mmoja kujifanya anamfahamu sana mume wa mtu.

"Mume wa mwenzio ulisimpakie wanja, mume wa mwenzio usijipitishepitishe, akikutongoza kataa, akikufuatafuata kamwambie mkewe." Mwisho wa kunukuu maneno kutoka kwenye wimbo huo.

Leo tunaiangalia filamu ambayo ina maudhui hayo.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa Bryan na mkewe Fatuma wanaishi vizuri. Lakini mwisho wa siku ndoa yao inaingiliwa na kidudumtu. Si mwingine ila ni Tifa.

Ni msichana mdogo, matata, jeuri ambaye alianza kutembea na Bryan mpaka mkewe akajua hilo.

Alimfuata na kumsihi amuache mumewe kwani wametoka mbali sana.

"Tifa wewe ni mwanamke mwenzangu, niliyoyapitia ni magumu mno wakati mwingine nagombana na mume wangu kwa sababu yako, kwa nini unataka kuniharibia ndoa yangu?"

Tifa akamjibu maneno mabovu yaliyomliza Fatuma na kuamua kuondoka zake alimwaga machozi njia nzima.

"Mumeo kanifuata mwenyewe, pweza hakai mbali na bahari.

Hata ungekuja na kigoma nisingekuelewa, mumeo simuachi na jeuri ya kuniacha mimi hana, unaona jinsi nilivyo, mtoto fulani hivi mweupe yaani mumeo ndivyo anavyotaka.

Sasa wewe na huo weusi wako kama kaniki, utegemee ulie machozi ukadhani mumeo nitamuacha sahau."

"He Ahsante" Akajibu Fatuma aliondoka huku analia, lakini alisindikizwa na maneno haya kutoka kwa Tifa.

Masikini analia, usilie mimi ni mke mwenzio, tugawane na kusaidiana majukumu"

Ndoa ikawa ndoana kwa Fatuma kwani mumewe akawa hasikii, haambiwi, haoni kwa Tifa.

Siku isiyo na jina, Fatuma alinyata nyumbani kwa kina Tifa na kuondoka na moja ya nguo zake zilizokuwa zimeanikwa kwenye kamba. Akaenda kufanya alichofanya. Tifa akawa kipofu.

Juhudi za kumponyesha zilishindikana. Bryan anaamua kurudi kwa mkewe. Miezi kadhaa baadaye Tifa akafariki dunia.





## MARAPA WALIOTIKISA KWENYE DANSI

**Na Adam Fungamwango**

KURAP kwenye muziki wa dansi kunatofautiana sana na kwenye muziki wa kizazi kipya. Marapa kwenye muziki wa kizazi kipya ni wale ambao wanaimba kwa kufokafoka, maarufu kama watu wa hip hop.

Asili yake ni nchini Congo DR, na ililetwa na bendi inayopendwa sana nchini humo Zaiko Langalanga. Hiyo ilisababisha bendi zingine ziige mfumo huo kutoka katika mziki ule wa rhumba ambao vyombo vinasikika peke yake bila maneno, na kuja ule ya mtu ambaye anasherehesha wakati ala zinapigwa, ndiyo huku kwetu Tanzania tukawaita marapa.

Marapa wawili wa Zaiko Langalanga, walikuwa wakisherehesha katikati ya muziki kwa kusema 'atalaku atalaku' na ndiyo maana nchini Congo DR, marapa hadi leo wanajulikana kwa jina la Atalaku.

Wakati Tanzania staili ya kurapu ikishamiri mwanzoni mwa miaka ya 2000, nchini Congo DR ilikuwepo ilishika kasi katikati ya miaka ya '80, lakini ikaja kuwa maarufu zaidi miaka ya '90 wakati wa bendi kama Sokouss Stars, Loketo Group, wanamuziki kama Yondo Sister, Kanda Bongo Man, lakini rapa maarufu ambaye hatasahaulika Tanzania na Congo DC ni Bileku Mpasi wa Empire Bakuba iliyokuwa ikiongoza na hayati Pepe Kalle.

Bendi kama Wenge Musica, Extra Musica, wanamuziki kama Koffi Olomide nao waliendeleza muziki wa kutumia marapa kiasi cha kupatikana kwa marapa maarufu kama, Robert Ekokota, Tutu Callugi, Theo Mbala na wengineo.

Hawa walisababisha kuwepo kwa marapa wengi nchini Tanzania kwenye bendi mbalimbali, wakinogesha muziki.

**1. Allan Mulumba Kashama**

Huyu ni Mkongomani, lakini alikuwa mmoja wa wanamuziki wa mwanzo kabisa Tanzania kufanya kazi ya kurap kwenye bendi za muziki wa dansi.

Akiwa na bendi ya Diamond Sound wana Dar es Salaam Ikindankoi alijipatia umaarufu sana kwa staili yake ya kurapu, 'amevaa kimini amevaa bodi suti'. Nyimbo kama "Neema', 'Kimalumalu' na zingine ambazo zilikuwa maarufu mno mwanzoni mwishoni mwa miaka ya '90 na mwanzoni mwa miaka ya 2000, zilimuweka kwenye chati ya juu na kuheshimika kwa kazi hiyo.

**2. Msafiri Diof**

Kwenye bendi ya African Stars 'Twanga Pepeta' kulikuwa na wanamuziki ambao walikuwa wakiimba, lakini pia wakimaliza kuimba wanarap, lakini hawakuwa marapa halisi.

Hao ni Banza Stone na Ally choki ambao kiasili si marapa bali ni waimbaji. Lakini kwa mara ya kwanza, Twanga Pepeta ilimpokea rapa halisi kutoka Kenya, Msafiri Diof, Mtanzania ambaye alikwenda kutafuta maisha na kuamua kurejea nchini.

Ni rapa kwa kiwango cha juu, amejipatia sifa kubwa akiwa kwenye bendi hiyo ambayo hadi leo badi yupo.

**3. Totoo Ze Bingwa**

Mwenyewe anajiita rapig mia saba sabini na saba katika siku saba. Huyu ni Mkongomani anayefanya kazi nchini na amepitia bendi mbalimbali za dansi kubwa zikiwemo FM Academia, Akudo Impact na zingine.

Ametoa mchango mkubwa wa muziki wa dansi, hasa kwenye staili ya kurap. Kwa sasa ana kundi lake la Sanaa Sana Band.

**4. Kalala Junior**

Ni mtoto wa mwanamuziki nguli nchini Hamza Kalala. Pamoja na kwamba Kalala Junior ni mwimbaji, lakini alianza muziki kama rapa na vile vile anakofanya vizuri zaidi na mashabiki wake wengi hupenda zaidi anavyorap. Amewahi kupitia bendi mbalimbali kama Bambino Sound. Mpaka sasa bado anaendelea na muziki.

**5. Khalid Chokoraa**

Kilikuwa kizazi fulani hivi cha pili cha marapa ambacho kiliibuka baada ya Ally Choki kwenda kuunda bendi ya Extra Musica. Nyimbo za bendi hiyo na aina yake ya kurap, ilitishia bendi nyingi za staili hiyo. Hadi leo amekuwa mmoja wa marapa bora kabisa nchini Tanzania.

# Yaliyomkuta Miss Zimbabwe hayavumiliki

MSHINDI wa Miss Universe Zimbabwe, Brooke Bruk-Jackson mwenye miaka 21, ameibua mtazamo mpya katika bara la Afrika baada ya raia wa nchi hiyo kudai hana hadhi ya kuwakilisha taifa hilo kwa kuwa ni mzungu.

Wengi hawakutarajia kuona watu weupe wakibaguliwa, lakini Zimbabwe imekuwa tofauti baada ya kuonekana ubaguzi huo wa rangi wakilengwa watu weupe.

Shindano hilo lilifanyika kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 22 wiki iliyopita, lilimalizika kwa hisia kali za kibaguzi hasa kwa watu weusi kuwaona wazungu si wenzao.

Washiriki wanawakilisha majimbo 10 ya taifa la Zimbabwe na ni pamoja na raia wa Zimbabwe wanaoishi ughaibuni.





## Naira Marley asisitiza hahusiki

MWANAMUZIKI Azeez Adeshina Fashola, maarufu kama Naira Marley, ameapa kurejea Nigeria kusaidia polisi katika uchunguzi unaoendelea kuhusu kifo cha Mohbad.

Mwimbaji huyo anatuhumiwa na mashabiki wa muziki kuwa anahusika na kifo hicho.

Marley alichapisha taarifa kwenye mtandao wa Instagram, akisisitiza haogopi kurudi nchini mwake kuhofia kukamatwa na aliendelea kukanusha kuhusika kwa namna yoyote na kifo cha Muhbad.

## Princess umefanya utafiti?

MSANII wa uchekeshaji kutoka Nigeria Damilola Adekoya, anayejulikana kama Princess, amesema nchi hiyo imejaa watu wanaonyanyasa na kuomba misamaha ya ubakaji.

Princess amesisitiza kwamba waathiriwa wengi wa ubakaji wako katika hatari ya kuwa wanyanyasaji wenyewe.

"Wanigeria wengi kwa kweli ni wabakaji na waombaji msamaha ya ubakaji. Hebu niambie, kati ya kila watoto 10 ambao wananyanyaswa, watano kati yao kama watageuka wanyanyasaji itakuwaje? Amehoji.





## Mkongwe wa Nolywood afariki dunia

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Pa Yemi Lawrence Adeyemi, aliyefahamika kwa jina la Saura, amefariki dunia.

Kulingana na Guardian Life, kifo chake kilitangazwa na mtoto wake Adetoun Adeyemi.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa alifariki dunia siku ya Jumapili, hata hivyo mazingira ya kifo chake hayakuwekwa wazi.

## Britney azua ugomvi

UGOMVI kati ya staa wa muziki nchini Marekani Britney Spears na dada yake Jamie Lynn, unazidi kuwa mbaya baada ya wawili hao kuonekana kuchuniana.

Mashabiki wa Britney wameingia mitandaoni na kufanya kampeni kubwa ya kumwangusha kisanii Jamie na mpenzi wake mcheza dansi Ilan Bersten.

Katika kitu ambacho dada wa mwanamuziki huyo kimemuudhi na kuamua kununa ni kitendo cha mpenzi wake kufananishwa na nyota wa Zoey 101.



# Katoliki Arusha lajivunia mafanikio lukuki

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KANISA Katoliki Jimbo Kuu Arusha limesema linajivunia uanzishwaji wa miradi ya kijamii, kukuza waumini wake kiroho na kiuchumi katika kipindi cha miaka 60 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1963.

Baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa hospitali tatu zilizopo Wasso wilayani Ngorongoro, Enduleni na ya Mtakatifu Elizabeth jijini Arusha maarufu kwa jina la kwa Babu.

Vilevile, ujenzi wa vituo vya afya zaidi ya saba, zahanati 13, shule za sekondari, msingi na awali.

Miradi ya misitu, mifugo, maji, kilimo na ndama mitamba, utoaji huduma kwa watu wenye ulemavu katika kijiji cha Olkokola wilayani Monduli na uanzishwaji wa kituo cha Uhai kwa ajili ya kutoa ushauri nasaha kwa waathirika wa Ukimwi.

Mafanikio mengine ni uanzishwaji wa kitengo cha CARITAS kinachoshughulikia kinga dhidi ya majanga yasiyozuilika katika jamii ambayo ni ukame, mafuriko na magonjwa ya milipuko.

Hayo yalisemwa jana na Aporinali Shiyo wa Ofisi ya Mawasiliano wa Jimbo hilo katika taarifa yake ya shughuli za maendeleo ya kiroho na kimwili yaliyofanywa jimboni humo ndani ya kipindi hicho.

Alisema kwa upande wa kiroho, elimu zimetolewa kwa vijana na watoto ili kuwaepusha na matumizi mabaya ya mitandao na kuwahimiza matumizi sahihi na yenye tija kwao.

Alisema mashirika ya kitawa yenye walimu wauguzi na madaktari, yaliongezeka jimboni humo na kuanzisha miradi ya afya na elimu.

Kwa mujibu wa Shiyo, mafanikio hayo yalifikiwa kwa haraka kutokana na ushirikiano baina ya kanisa na serikali.

Alisema kwa kipindi hicho, jimbo hilo limeongozwa na maaskofu wanne, ambao ni marehemu na vipindi vyao kwenye mabano Mhashamu Askofu Dennis Vincent Durning (mwaka 1963 hadi 1988) na Askofu Fortunatus Lukanima (1985-1997).

Askofu Mkuu Mstaafu Josephat Lebulu (1999-2017) na Askofu Mkuu Isaac Amani (2018-2023), ambaye katika uongozi wake amejikita kusimamia maadili kwa watoto na vijana, kuhimiza umuhimu wa jamii kujitambua, kuwajibika, kuimarisha imani na kudumisha ushirikiano kila mmoja.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza, Cuthbert Midala (wa pili kushoto), akikagua madarasa manne na ofisi mbili zilizojengwa kwa nguvu za wananchi na Mgodi wa Sotta kwenye Shule ya Sekondari Lubungo, katika kijiji cha Lubungo, mapema wiki hii. Kushoto ni Ofisa Mkuu wa Fedha wa Kampuni ya Sotta Mining, Isaac Lupokela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataalamu maabara 'walia' mitaala inawakanganya

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WATAALAMU wa maabara nchini wamesema wanakabiliwa na tatizo la tofauti wa mitaala inayotolewa na vyuo vikuu nchini na kusababisha mkanganyiko kwenye muundo wa utumishi.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Rais wa Chama cha Wataalamu Wanasayasi wa Maabara, Yahaya Mnunga.

Mnunga alisema kuwa kuna vyuo vinavyofundisha ngazi moja ya elimu kwa miaka mitatu na vingine minne na kuleta mkanganyiko kwenye soko la ajira hususani muundo wa utumishi ndani na nje ya nchi.

"Tunaiomba serikali kuangalia upya jambo hili, ikiwa ni miaka mitatu kwa shahada ya kwanza basi ifanyike hivyo, na ikiwa ni miaka minne ifanyike hivyo, hii itasaidia kuleta usawa katika muundo wa utumishi," alisema na kuongeza kuwa:

"Pia lipo tatizo la udahili kwa wataalamu wanaokusadia kujiendeleze kwenda shahada ya kwanza, hii ni kutokana na mwaka 2015 sifa za kujiunga kutumia vigezo vya zilibadilishwa kutoka GPA2.7 mpaka 3 jambo ambalo linawafanya baadhi licha ya kuwa wafanyakazi kwa bidii hawawezi kujiendeleza, tunaomba serikali pia iangalie hili. " Akifungua kongamano hilo, Naibu Waziri wa Afya, Dk Godwin Mollel alisema chagamoto hizo wamezopkea na kuahidi kuzifanyia kazi kwa kushirikiana na viongozi na wadau wengine wa afya

"Kukutana kwao hapa kumesaidia kuzungumza matatizo mbalimbali yanayowakabili, sekta hii ni muhimu sana na ni moyo wa hospitali yoyote, sisi kama wizara kwa kushirikiana na wadau wa afya tutahakikisha tunamaliza matatizo haya," alisema Dk Mollel.

Baadhi ya wananchi wa Manispaa ya Moshi, akiwemo Maria Msofe alisema bado kuna matatizo katika kada hiyo kutokana na kupewa majibu tofauti kwa baadhi ya magonjwa hasa yatokanayo na mkojo.

"Hili la mitaala inawezekana ni sababu ya kutofautiana kwa majibu, tunaomba serikali kuliangalia na kufuatilia kwa kina katika vituo vya afya ili huduma bora zitolewe kwa wananchi," alisema Zaina Hasan.

Nchini kuna vyuo vipatavyo 52 vya afya.

# Watoto wenye VVU waongezeka, wapungua Manyara

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

IDADI ya watoto chini ya miaka mitano wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) mkoani Manyara inaongezeka na kushuka kila mwaka kutokana na baadhi yao kuhama na kushindwa kupelekwa vituo vya afya kupata huduma.

Akizungumza na Nipashe juzi Mratibu wa kudhibiti UKIMWI mkoani humo, Charles Shija, alisema mwaka 2020 walikuwa watoto 160 mwaka 2021 watoto 163 na mwaka huu hadi kufikia Juni watoto 159.

Shija alisema idadi hiyo inaongezeka kidogo kidogo na kushuka kwa kuwa wengine wanavuka nao kila mwaka.

Alisema chanzo cha ongezeko kuwa dogo ni baadhi ya watoto kuhama bila ya wazazi na walezi kutoa taarifa na wengine kuvuka umri.

Alisema licha ya elimu kupewa msisitizo mkubwa dhidi ya Ukimwi, lakini wamekuwa wakikabiliwa na vikwazo hivyo.

Mratibu huyo, alisema watoto hao wanapelekwa kliniki za VVU na wazazi na walezi wao.

Mkurugenzi wa Shirika la Baraka Community Concerns Foundation, Jovin Riziki, alisema watoto wengine wanakosa huduma za kupata dawa za kufubaza VVU kutokana na hali ngumu ya maisha na vituo vya afya kuwa mbali na maeneo wanakoishi.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2022 nusu ya watoto wenye VVU wanapokea dawa za kurefusha maisha.

Akizungumzia kuhusu tatizo hilo, Mkazi wa Mtaa wa Hangon A, Elizabeth Msuya aliitaka serikali na wadau kuendelea kutoa elimu ya umuhimu kwa waathirika kutumia dawa hizo na kudhibiti maambukizi mapya katika jamii.

Mkazi wa Babati, Paul Ezekiel, alisema kwa kuwa watoto ni tegemeo kwa Taifa ni vizuri wenye VVU wakapewa huduma stahiki kwa manufaa ya baadaye.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# 'Guruwe' na 'mtumba', magari 504 fahari enzi hizo kama leo VX na V8

**Na Adam Fungamwango**

SARA acha majivuno, usiwe kama Mwanaisha kanikataa kwa kuwa mimi ni mshona viatu. Kampata, mshikaji mwingine hehehe, mwenye gari kubwa sana 'mtumba', kavunja unyuma Mwanaisha sababu ya bwana mwenye gari.

Hiki ni kipande cha wimbo uliopigwa na bendi ya Urafiki Jazz miaka ya mwanzoni mwa 1980. Unaitwa 'Sara Acha Majivuno', ukitungwa na kiongozi wa bendi hiyo, Juma Mrisho 'Ngulimba wa Ngulimba.'

Maudhui ya wimbo huu ni kwamba kuna msichana anaitwa Mwanaisha ambaye alimkataa mwanaume anayefanya kazi ya kushona viatu kwa sababu ya mwingine mwenye gari aina ya 'mtumba.'

Kabla hatujaenda mbali sana, hapa ndiyo inadhihirisha kuwa siyo siku hizi tu ambapo baadhi ya wanawake wanatuhumiwa kuwakataa wanaume wasio na kitu bali hata zamani jambo hili lilikuwepo. Mnawaonea tu masistaduu wa kisasa. Kumbe baadhi ya mama na bibi zao walikuwa hivyo hivyo.

Twende sasa kwenye mada husika. Tumesikia hapa gari la 'mtumba.' Haya ni magari yaliyoingia na kuvuma sana hapa nchini katikati ya miaka ya 1970 hadi mwishoni mwishoni mwa miaka ya 1980 yalipoanza kupotea taratibu, lakini pia kupitwa na wakati.

Kwa wakati huo ndiyo yalikuwa magari ya kifahari na yeyote aliye nalo akaheshimiwa na kuonekana ni mmoja wa watu wenye fedha, na hata dereva tu anayeliendesha akabeba heshima eneo lote analoishi mtaani.

Ni kama sasa hivi tu mtu amiliki gari aina ya Toyota VX au V8, au hata dereva wake tu anavyoheshimika.

Kwa sasa aina hii ya magari hawezi kuwa nayo mtu wa kawaida, badala yake mmiliki wake ni lazima awe mtu mzito, na kwa kiasi kikubwa zinamilikiwa na serikali na kutumiwa na Mawaziri, Wabunge, Wakurugezi, Wakuu na Mikoa na watumishi na ngazi mbalimbali za serikali.

Ilikuwa kama hivyo zamani magari hayo yalikuwa yakimiliwa na serikali, mabalozi wa nchi mbalimbali waliopo nchini, Taasisi za Kidini na mashirika machache ya umma lakini ni mabosi tu walikuwa wakiendeshwa kwenye magari hayo.

Watu binafsi pekee wachache waliokuwa nayo ni wale tu ambao walikuwa wamekwenda nchi za ng'ambo, Ulaya na kurejea wakiwa mambo safi.




Gari aina ya Peugeot 504, maarufu kama 'mtumba' au 'guruwe' iliyotikisa katikati ya miaka ya 1970 hadi mwishoni mwa 1980.

Mbali na kuitwa 'mtumba', lakini vile vile yalikuwa na majina mengi, huku watoto wa mjini wakilipachika jina la 'guruwe'. Kama baadhi walivyolibatiza gari aina ya Noah sasa hivi.

Magari haya yaliyotisha kipindi hicho yaliitwa Peugeot 504. Pamoja na kwamba Kampuni ya kutengeneza magari ya Peugeot ilitengeneza aina nyingi ya magari yaliyoingia nchini na kutamba, lakini gari aina ya 504 iliondokea kupendwa na ya kiwango cha juu, ikibeba ishara ya fahari ya kipesa, ikiwa na bei juu kuliko nyinginezo.

Hapa Tanzania walikuwa na eneo lao la kuuzia magari, kwa wanaolijua jiji la Dar es Salaam, ni pale zinapokutana barabara tatu, itokayo Maktaba Kuu ya Taifa na nyingine inayoungana nazo kuelekea Hoteli ya Serena, Royal Palm, au sijui vile siku hizi Movenpick Royal Palm! Na ya tatu ile inayokwenda Daraja la Salenda.

Katikati ya miaka ya 1970 lilitokea kundi lingine la walioenda ughaibuni, nao katika kujitutumia mimi ni nani, wakarejea nchini na Peugeot 504.

Hata hivyo, zao zilikuwa tofauti kidogo, usukani wake ulikuwa upande wa kushoto, juu kulikuwa na sehemu ya kufungua kiasi kwamba mtu aliyekuwa ndani anaweza kusimama, kuchungulia na ndivyo wenye nazo walitamba nazo sana ufukweni mwa bahari kama Coco Beach, na ufukwe wa Kurasini enzi hizo kunaruhusiwa.

Wamiliki wake, kwa kiasi fulani walitawaliwa na hilo kundi la waenda nje, akijulikana hasa kwa jina la mabaharia, huku hayo magari yao yaliitwa 'mitumba.' Kwa maana hii hii tunayoijua leo. Tofauti ndogo ya sasa na enzi hizo ni kwamba haikuruhusiwa mitumba ya aina yoyote ya ndani ya nchi, iwe mavazi hadi mashine.

Hata hivyo, hizo 504 ni kizazi cha katikati ya miaka ya 1970, maana historia inaonyesha magari ya Peugeot kutoka Ufaransa yana ukongwe wa miaka 213, tangu kampuni kuasisiwa, kila baada ya miaka michache linatoka toleo lingine.

Kwa zama zetu, kuanzia miaka ya 1960 nchi ikiwa nchi ikiwa mbichi kutoka kwenye plastiki begi yake, ilitamba sana gari aina ya Peugeot 403, zikianza na aina ya ambazo mlango wake unafunguliwa kwa kinyume na tulivyozoea leo, huku sauti yake ni kama inakubembeleza gari inapotembea.

Baadaye zinafuatiwa na 404 zikizotawala mno, zikiwemo taxi za mjini, kabla ya gwiji 504 kuibuka katikati ya 1970.

Baadaye ziliibuka 305, 304, 402, zikiwa katika staili zinazofanana kuchongoka nyuma na mbele pana, lakini hazikumudu kuipiku 504 kwa miaka yote ya kuvuma kwao, kabla ya kupinduliwa sokoni na magari ya Kijapani, kabla ya ofisi za Peugeot Dar kutoweka kabisa nchini.

Kampuni inayotengeneza magari hayo iliazishwa nchini Ufaransa mwaka 1810 na mbwanyenye mmoja anaitwa Armand Peugeot, ina maana magari hayo yaliitwa kwa jina la mmiliki wake.

**Tuma meseji 0716 350534**



Aina nyingine ya Gari ya Peugeot 504, iliyoundwa na staili tofauti na ya kwanza. Hii iliitwa 'station Gagon', au 504 family kama ilivyokuwa ikiitwa na watoto wa mjini.

## HABARI KIMATAIFA

# Putin amteua kiongozi Wagner kusimamia mapigano Ukraine

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin amekutana na mmoja wa makamanda wakuu wa zamani wa kundi la Wagner, ambaye kwa sasa anafanya kazi katika wizara ya ulinzi ya nchi hiyo.

Kamanda huyo Andrei Troshev alikuwa msaidizi wa zamani wa kundi hilo lililoongozwa marehemu Yevgeny Prigozhin, ambaye aliuawa katika ajali ya ndege mwezi Agosti.

Kifo chake kilikuja miezi miwili baada ya wanajeshi wa Wagner kuonyesha uasi kwa kuandamana kwa muda mfupi kuelekea mji mkuu wa Moscow.

Taarifa ya Ikulu ya Kremlin ilisema Rais Putin alimwomba Troshev kusimamia vitengo vya wapiganaji wa kujitolea wanaopigana nchini Ukraine.

Akizungumza na Troshev, rais huyo alisema anaweza kushirikiana kwa karibu na vitengo vya kujitolea vinavyoweza kufanya kazi mbalimbali katika mapigano.

"Unajua kuhusu masuala ambayo yanahitaji kutatuliwa mapema ili mipangilio katika eneo la mapigano iende kwa njia bora na yenye mafanikio," alisema Putin.

Msemaji wa Kremlin Dmitry Peskov aliambia shirika la habari la RIA kwamba Troshev sasa anafanya kazi katika wizara ya ulinzi.

Mkutano huo unawadia wakati Rais Putin akijaribu kuhakikishia mamlaka yake kufuatia maasi ya Wagner mwezi Juni.

Katika muda wa saa 24 pekee, Prigozhin alifanya uasi, na kutuma wanajeshi katika mji wa kusini wa Rostov, kisha kuahidi kuelekea Moscow, kabla ya kurudi nyuma.

Uasi huo ulikuwa changamoto zaidi kwa mamlaka ya Putin katika miongo miwili.

Mwezi uliopita, kiongozi huyo alitoa wito kwa wafanyakazi wote wa Wagner na wakandarasi wengine wa kijeshi wa kibinafsi wa Russia kula kiapo cha utii kwa serikali ya Russia. Wakati huo huo Russia jana iliadhimisha kumbukumbu ya mwaka mmoja tangu iliponyakua majimbo manne ya mashariki na kusini mwa Ukraine.

Kumbukumbu hiyo iliambatana na tamasha litakalofanyika katika uwanja wa kihistoria wa Red Square, mjini Moscow, ambalo linalenga kutambulisha umma siku mpya ya mapumziko itakayokuwa ikiadhimishwa nchini humo kila mwaka.

Hata hivyo, vikosi vya Russia havidhibiti kikamilifu majimbo ya Kherson, Zaporizhzhia, Donetsk na Luhansk, na vimelazimika wakati mwingine kusalimisha maeneo kadhaa kufuatia mashambulizi ya Ukraine.

Makabiliano baina ya Russia na Ukraine yanaendelea kuripotiwa sehemu mbalimbali ya nchi hiyo.

Idara ya ulinzi wa anga ya Russia ilisema imeziharibu ndege 11 zisizo na rubani zilizorushwa na Ukraine katika maeneo ya Kursk na katika mkoa wa Kaluga takriban kilomita 200 kusini-magharibi mwa mji mkuu wa Moscow.

**BBC**



Wakimbizi kutoka mkoa wa Nagorno-Karabakh wakisubiri kuingia nchini Armenia kunusuru maisha yao. **PICHA: AP**

# Kagame amteua mwanajeshi anayetuhumiwa kuwa waziri

**KIGALI,** RWANDA

RAIS wa Rwanda Paul Kagame amemteua Ofisa Mkuu wa Kijeshi kuwa waziri wa nchi wa ushirikiano wa kikanda.

Jenerali James Kabarebe anashutumiwa kufanya kazi kwa karibu na kundi la waasi la M23 linalofanya mashambulizi katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Miongo kadhaa amekuwa mshirika wa karibu wa Rais Kagame, alistaafu kutoka jeshi mwezi uliopita. Wataalamu wa Umoja wa Mataifa walichapisha ripoti mwezi Juni wakimtuhumu Jenerali Kabarebe kwa kuwa na jukumu kubwa katika kuratibu operesheni za kundi la waasi la M23 mashariki mwa DRC. Rwanda imekanusha kuwa jeshi lake limeunga mkono kundi la M23.

Tangu kundi hilo lianzishe tena uasi karibu miaka miwili iliyopita, mamia ya maelfu ya raia wamelazimika kuyahama makazi yao.

**BBC**

## Watu 85,000 wakimbilia Armenia

**NAGORNO,** ARMENIA

WATU 85,000 wameomba hifadhi nchini Armenia baada ya Azerbaijan kuudhibiti mkoa unaozozaniwa wa Nagorno-Karabakh.

Shirika la Kuwahudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) lilisema idadi hiyo itaongezeka kutokana na kasi ya watu kuhama makazi yao katika eneo hilo. Msemaji wa serikali ya Armenia, Nazeli Baghdasaryan, alisema idadi hiyo ya watu ni wale waliolazimishwa kukimbia makazi yao katika mkoa huo.

Kulingana na taarifa ambazo hazijathibitishwa, Waarmenia wapatao 120,000 wameingia katika nchi hiyo ambao awali walikuwa wakiishi katika mkoa wa Nagorno-Karabakh.

Azerbaijan ilifanya mashambulizi mapema wiki hii na kufanikiwa kudhibiti kamili mkoa huo ambao umezozaniwa kwa miongo kadhaa.

Serikali isiyotambuliwa ya Artsakh iliyokuwa ikiongoza jimbo hilo ilitangaza wiki hii kuwa itahitimisha uwepo wake kuanzia Januari Mosi mwaka ujao.

Waarmenia waliokuwa wakiishi katika mkoa huo, wamekuwa na hofu ya kuteswa na uwepo wa vurugu kutoka upande wa Azerbaijan.

Waziri Mkuu wa Armenia Nikol Pashinyan aliishutumu jirani yake Azerbaijan kwa kampeni yake ya kijeshi inayolenga ukabila.

"Uhamaji wa Waarmenia kutoka Nagorno-Karabakh unaendelea kutokana na sera ya safisha safisha ya kikabila ya Azerbaijan. Uchambuzi unaonyesha kuwa katika siku zinazokuja hakutokuwa na raia hata mmoja wa Armenia atakayesalia," alisema waziri mkuu Pashinyan.

**DW**

## Watu 52 wauawa kwenye mlipuko

**KARACHI,** PAKISTAN

WATU 52 wameauwa na wengine zaidi ya 50 wamejeruhiwa nchini Pakistan katika shambulio la kujitoa mhanga.

Shambulio hilo lilitokea jana wakati wa sherehe za kidini huko Mastung katika mkoa wa kusini magharibi wa Baluchistan, wakati waumini wa Kiislamu wakisherehekea kuzaliwa kwa Mtume Muhammad.

Naibu Inspekta Jenerali wa Polisi eneo hilo Munir Ahmed aliliambia shirika la habari la Reuters kuwa mshambuliaji alijilipua karibu na gari la Naibu Msimamizi wa jeshi la Polisi lililokuwa limeegesha karibu na msikiti ambao ulianguka na kuwafukia chini ya vifusi watu.

Hakuna kundi lililodai kuhusika na mlipuko huo ambao umetokea kukiwa na ongezeko la mashambulizi ya makundi ya wapiganaji magharibi mwa Pakistan.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**RAHABU LUCAS PAUL** anatangaza kupotelewa na kadi za magari aina ya **RAV4** yenye namba za usajili **T.374 DUQ na HIACE** yenye namba za usajili **T.331 DYM.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya Polisi. **PHQ/GEI/MBO/921/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ZUWENA HAMISI BAKARI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina aina ya **SINORAY** yenye namba za usajili **MC 246 CXF.** Chassis No. **LD3PCK6J3M2004714,** Engine **NO. sr162fmj21004714.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/410258/2022.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KIWANJA

**ALLY MOHAMED KHERI,** Anatangaza kupotea kwa Hati ya kiwanja yenye Jina la Umiliki AMINA MBARAKA ALLY Kiwanja kipo BAHI ROAD HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA Yenye **PLOT NO 80, BLOCK B' BAHI ROAD DODOMA CITY COUNCIL.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **DOD/DOD/RB/185099/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LEWIS MICHAEL MPANGALA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SUBARU FORESTER** yenye usajili namba **T 138 DFD , CHASSIS NAMBA: SG5014764** na **ENGINE NAMBA: EJ20B593936.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **KAB/RB/2427/2023**

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI ILIYOPO SHINYANGA**

**SHAURI LA MAMLAKA YA ZIADA**

**SHAURI LA MAOMBI YA ARDHI NAMBA 06 YA 2022**

1) MAXIE SONDO
2) JOHN BUTONDO
3) BLANDINA GOGADI..............................MDAI

**DHIDI YA**

1) BARAKA MIGERA
2) HAMPHLEI KIMARO......................WADAIWA

SHAURI LIMEPANGWA KUSIKILIZWA MNAMO TAREHE 02/10/2023 SAA 3.00 ASUBUHI KATIKA MAHAKAMA YA MKAZI SHINYANGA NA UNATAKIWA KUWEPO, AU KUWAKILISHWA KISHERIA PAMOJA NA KULETA UTETEZI WAKO DHIDI YA MAOMBI HAYA.
ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWAKO TAREHE HIYO, SHAURI LITAANZA KUSIKLIZWA BILA WEWE KUTAARIFIWA TENA NA MAAMUZI KUTOLEWA.
IMETOLEWA KWA MKONO WANGU NA MHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 18/09/2023.

**HAKIMU MKUU MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**SHINYANGA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**

**ILIYOPO WILAYA YA MOROGORO**

**SHAURI LA MAOMBI MADOGO NA. 40/2023**

**ENOCK PETER: ....................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**EMMANUEL REMY MAHWISA:............MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**
**EMMANUEL REMY MAHWISA**
**POPOTE ULIPO**

Unatakiwa ufike katika Mahakama ya Wilaya Morogoro tarehe 09/10/2023 saa 2:30 asubuhi ambapo shauri lako limepangwa kutajwa.
Endapo hutofika wewe binafsi ama mwakilishi wako shauri tajwa litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
Imesainiwa leo tarehe 18 Mwezi 09 mwaka 2023

T. KANIKI
HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MOROGORO

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE INCHARGE DISTRICT COURT P.O. Box 660, Morogoro

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 170 YA 2023**

**TANZANIA RAILWAYS CORPORATION: ...MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**PILI HAMADI SALEHE (MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU ALLY CHANDE)**
**ALLY S. KAZIMIRI, OMARY HAMISI, EVANCE AMLIMA, WILBROD S. LEMAU, HEMEILI S. KINYOGOLI, STUMAI KAZIMIRI....................................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**WILBROD S. LEMAU**
**HEMEILI S. KINYOGOLI**
**STUMAI KAZIMIRI**

Popote mlipo mnaarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 5/10/2023 mbele ya Mwenyekiti M. Khasim ninyi wenyewe binafsi au mtume wawakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 26 mwezi September, 2023.

M. KHASIM
MWENYEKITI

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MOROGORO TANZANIA

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO.94 OF 2023**

**IN the Matter of the late ELIREHEMA CANHAM KILEO**

**By 1.EVALINE WARIAEL URIO**
**2.............................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 23/10/2023.

Dated at Morogoro this 25 day of 09 2023.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA KINONDONI**
**KINONDONI**

**MAOMBI MADOGO NA. 20/2022**
**(yametokana na shauri la mirathi no 95/2020 mbele ya Mh. Lyamuya, mirathi ya marehemu Asha Rajabu Msekeni)**

**PELLEGREEN JUMA MKANA ......................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JOYHEFSIBA JUMA KILLO......................MJIBU MAOMBI**

**Kwa:**
**JOYHEFSIBA JUMA KILLO**
**DAR ES SALAAM.**

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi ambayo maelekezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii wewe binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anayeruhusiwa siku ya Alhamisi tarehe 05 mwezi 10 mwaka 2023 saa tatu (9:00) kamili asubuhi. Kwa kuwa siku hiyo ni kutajwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na maombi haya.
**ANGALIA**
Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila ya uwepo wako.

RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM
**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA KINONDONI/KIVUKONI**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 444 LA 2023**

**SAMWEL YOBU MEENA NA WENGINE 2.....MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ELIA HERGARD SAM'....................MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**ELIA HERGARD SAM'**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**SAMWEL YOBU MEENA NA WENGINE 2** wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 2/10/2023 saa 3:00 AM Asubuhi/mchana mbele ya Mh **J.W.SILLAS** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 19 Mwezi 09,2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa bianadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-28

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

“Mpenzi nikwambie kitu, kuna wanaume wabaya sana duniani. Mimi nilikuwa ni mpenzi wa Charton, yaani mchepuko wake, huku yeye ana mke ambaye ndiyo huyo marehemu Tessy.

Kilichotokea ni kwamba Rukia alimpelekea Charton picha moja ambayo ndiyo imeleta maafa yote hayo.

Hiyo picha ya mnato, ni ya mwanaume mmoja amepiga na Tessy. Baada ya hapo ndipo Charton alipoanza kumuwinda mkewe taratibu na kumuua baadaye bila ya kushtukiwa na mtu yeyote. Hadi leo yupo mtaani nadhani alijipanga. Huyo mwanaume naye alisakwa nakwambia kama mhaini lakini hakupatikana. Na baada ya mazishi kupita na nini, aliyempelekea picha ndiyo akaonekana wa maana, mimi nikapigwa chini akachukuliwa yeye.” Akashusha pumzi nzito.

“Du! Kumbe ndiyo hivyo?” Eddy akajifanya kushangaa kama vile hajui nini kinaendelea.

“Sasa hiyo picha ilipelekwa ili Tessy aachwe, auawe au iwe vipi?”

“Enhee, hapo umeenda kule kule, unajua Rukia na Tessy walikuwa marafiki tangu wanasoma shule ya sekondari habari nilizozipata kwa waliosoma nao ni kwamba Rukia alimpenda sana Charton na alitaka yeye ndiye aolewe, lakini halikutokea bahati ikamuangulia Tessy, kumbe mwenzake aliliweka rohoni kwa miaka mingi.

Ikapatikana sababu ya hiyo picha ikapelekwa kwa mwanaume ili amuache na kumuoa yeye, lakini Charton akaamua kufanya alivyofanya. Sasa ni kweli kwa sasa ni wapenzi wataoana hivi karibuni lakini wote wawili wametapakaa damu mikononi.

“Huyo mwanaume ambaye alipiga picha na Tessy ni nani?”


“Ni Barton!”

“Ni kweli walikuwa na uhusiano naye wa kimapenzi?”

“Ni kweli, lakini ilikuwa zamani!”

Jibu hilo likashtua na kumchanganya kidogo Eddy.

“Nikwambie mpenzi Denis, nikwambie tu kuwa yule Rukia ni mwanamke mbaya sana, yeye ndiye chanzo cha yote na anajua hilo, sasa alichotaka amekipata. Mwenzake amekufa, yeye ndiye anakwenda kuolewa.”




“Na wewe mchepuko wa mume wa Tessy umeachwa!” Akadakia Eddy.

“Bwana wee! Akajibu Nancy, lakini kwa sasa sijali sana kuhusu hilo, nipo na wewe!”

“Enhee tuendelee, kuna neno hapo ulisema walikuwa wapenzi, lakini ilikuwa zamani, ina maana hadi picha inapelekwa kwa Charton walikuwa wameshatengana?” Akazidi kudodosa.

Nancy alitiririka akiwa hajui kabisa kuwa anaongea na mpelelezi maarufu nchini na Afrika nzima aliyepewa kazi ya kuchunguza kifo cha mwanamke huyo huyo na alikuwa kwenye hatua za mwisho kabisa kukamilisha upelelezi.

Hakujua hata hayo anayoyaeleza ni moja kati ya mambo yaliyokuwa muhimu kabisa kwenye upelelezi wa Eddy. Na hata kuwa pale ilikuwa kwa sababu hiyo.

**“Ndiyo hivyo ili mke aachwe aolewe yeye kwa sababu alikuwa anataka hivyo tangu mwanzo.”**

“Kifupi tu mpenzi, ile picha ni ya zamani sana kabla Tessy hajaolewa na Charton.”

Eddy alishtuka, lakini kimoyomoyo bila Nancy kutambua. Sasa kuna kitu kingine alianza kukigudua.

“Historia inaanza nyuma, Tessy kabla ya kuolewa alikuwa na mpenzi wake Barton, na ile picha walipiga kipindi hicho. Lakini baadaye waliachana kila mmoja kivyake, na miaka mingi baadaye ndiyo akaonana na Charton wakawa wapenzi kabla ya kuoana. Lakini kwa Rukia hakupenda mwenzake Charton alitaka yeye ndiye aolewe badala ya rafiki yake. Akakasirika. Alitumia njia mbalimbali kuifanya ndoa ile iwe mashakani lakini alishindwa.

Katika pitapita zake kwa mashoga zake akakutana na picha hiyo ya zamani ya Rukia na Barton, akaona ndiyo hapa hapa. Akaichukua na kuipeleka kwa Charton. Akamdanganya na kumuaminisha kuwa ni picha ya hivi karibuni, kumbe ya miaka zaidi ya kumi iliyopita.”

“Sasa mpenzi, kama picha ilikuwa ni ya zaidi ya miaka 10, ina maana hakukuwa na kitu chochote kilichomfanya Charton kufahamu kuwa haikuwa ya sasa?”

“Kilichotokea ni kwamba, wakati Tessy anapiga picha na Barton alikuwa amenawiri, amenenepa, amependeza na alivaa gauni la maua maua, walipoachana alipungua sana.

Charton hakuwahi kumuona Tessy akiwa amenenepa na kunawiri huko nyuma, alikutana naye alikuwa amepungua sana, na amekuja tena kunenepea kwake na kunawiri.

Kwenye ile picha ilionyesha Tessy yule aliyekuwa amependeza na kunawiri kabla Charton. Haikuwezekana kushawishi Charton kumwambia ile picha ni ya zamani. Hajawahi kuona mkewe vile zamani, yeye alijua tangu zamani mkewe ni kimbaumbau, kwa hiyo moja kwa moja akajua ni picha mpya na ndivyo Rukia alivyotaka iwe vile.”

Eddy alikaa kimya na kutafakari bahati mbaya aliyoipata mwanamke huyo aliyeitwa Tessy ambaye alikatwakatwa kama nyama buchani.

“Ina maana Charton amemuua mkewe kwa kudanganywa tu na huyo mwanamke anayeitwa Rukia?”

“Ndiyo hivyo ili mke aachwe aolewe yeye kwa sababu alikuwa anataka hivyo tangu mwanzo.”

“Enhee nimesahau, pia mwezi mmoja tu kabla ya kuletewa hiyo picha, mwanamke alinunua gauni linalofanana sana na lile alilovaa. Mume alipoiona akajua ni picha mpya, wajihi wa mkewe na lile gauni. Nasikia Charton kwa ukatili wake hata hakumwambia kitu chochote mkewe. Nadhani labda angekaa naye na kumuuliza mkewe angeweza kumuonyesha vitu mbalimbali kwenye hiyo picha vinavyoonyesha ni ya zamani, lakini mwenyewe akapanga mpango huo wa kumuua bila kumwambia kitu. Kwanza alituma watu kumsaka Barton kimya kimya hawakumuona, ndiyo akafanya mauaji yake kwa mkewe.”

“Sasa mpenzi kwa nini hili usiende kulisema polisi ili jamaa akakamatwa?” Eddy alichombeza.

“Weee! Unamjua yule jamaa! Kuna baadhi ya maafande wako mikononi mwake, ana pesa mtu kama mimi si naweza kufagiliwa mbali, nikafa na mimi maiti yangu ikatupwa baharini ndugu zangu wakakosa hata mwili wa kuuzika!” Akajibu na kumfanya Eddy kuangua kicheko.

Kwa maelezo hayo tayari Eddy alipata mtuhumiwa mwingine ambaye ni Rukia. Yeye ndiyo chanzo cha mauaji. Kumshawishi Charton kuamini mkewe ni mzinzi kwa ajili ya kiu yake ya mapenzi.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# DAR CITY YATWAA UBINGWA KIKAPU KWA WANAUME DAR

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Dar City kwa upande wa wanaume imetwaa ubingwa wa kikapu mkoa wa Dar es Salaam baada ya kuifunga JKT vikapu 69-63 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Don Bosco uliyoko Upanga, Dar es Salaam juzi usiku.

Robo ya kwanza Dar City ilikuwa nyuma kwa vikapu 11-18 dhidi ya JKT, robo ya pili ilimalizika kwa timu hizo kufungana vikapu 33- 33 wakati robo ya tatu Dar City ilifunga JKT vikapu 51-42.

**Kutokana na kutwaa ubingwa huo, Dar City imezawadiwa kikombe pamoja na medali.**

Nafasi ya pili katika ligi hiyo imeshikiliwa na JKT Stars ambao walipata zawadi ya Sh. 500,000 pamoja na medali huku Pazi waliomaliza katika nafasi ya tatu wameondoka na Sh. 300,000.

Kwa upande wa wanawake, Vijana Queens ndio waliibuka mabingwa na wamepata zawadi ya Sh. milioni moja huku JKT Stars waliopewa Sh. 500,000 walimaliza wapili na Polisi iliyopata Sh. 300,000 ilishika nafasi ya tatu.

Hata hivyo Tumaini Ndosi wa Vijana Qeens alitangazwa kuwa Mchezaji Bora kwa upande wa wanawake huku Tairon Edward wa UDSM pamoja na Ally Faraji wa Dar City walitangazwa kwa upande wa wanaume.

Kocha Mkuu wa Vijana Queens ya wanawake, Kabola Shomari na Mohamed Mbwana wa Dar City (wanaume ) walitangazwa kuwa makocha bora katika ligi hiyo.

Akizungumzia ushindi huo Kocha Mkuu wa Dar City (Wanaume), Mbwana alisema ushindi huo umetokana na maandalizi ya muda mrefu waliyoyafanya.

"Tumefurahi kupata ubingwa, haikuwa kazi rahisi , katika fainali tumekutana na timu yenye wachezaji wenye uzoefu, ninawapongeza sana wachezaji wangu kwa kufuata mbinu na maelekezo mbalimbali niliyowapa," alisema Mbwana.




Wachezaji vijana wanaofundishwa katika Kituo cha Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kilichoko Mnyanjani, Tanga wakifanya mazoezi ili kukuza vipaji vyao. **PICHA: TFF**

# Chipukizi yaisimamisha KMKM

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

BAADA ya timu yake kupoteza mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar, Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu amesema matokeo hayo yametokana na ushindani mkali waliopata kutoka kwa wapinzani wao, Chipukizi.

KMKM ambao ndio mabingwa watetezi walikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Chipukizi katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Finya, uliokoPemba juzi.

Msimu aliliambia gazeti hili wachezaji wake walicheza vizuri na kwa kufuata maelekezo lakini bahati haikuwa upande licha ya jitihada walizoonyesha katika mchezo huo.

Kocha huyo alisema mchezo huo ulikuwa mgumu tangu awali na wapinzani wao walijipanga kupata matokeo chanya baada ya kufanya vibaya katika michezo yao mitatu iliyopita.

"Tumepoteza ugenini, wachezaji walicheza vizuri na walijitahidi kuzuia mashambulizi na kuzitumia vizuri nafasi tulizopata lakini niseme tu bahati haikuwa yetu, hivyo mchezo huu tumepoteza sasa tutajipanga kuelekea mchezo unaofuata," alisema Msimu.

Aliongeza wanaenda kurekebisha makosa kwa ajili ya kuingia wakiwa imara katika mechi yao inayofuata dhidi ya Ngome FC itakayochezwa Oktoba 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Mau A.

Ligi Kuu Zanzibar inatarajia kuendelea tena leo kwa Maafande wa KVZ kuwakaribisha Kundemba FC kwenye Uwanja wa Mau A huku kwenye Uwanja wa Mau B, Uhamiaji FC watavaana na Kipanga.

# Daraja la Kwanza Unguja Oktoba 2

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

NEW boys wanatarajia kuikaribisha Raskazone katika mechi ya ufunguzi ya Ligi Daraja la Kwanza itakayochezwa Oktoba 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kichakanyuki huku Shangani wakiivaa Paje Star kwenye Uwanja wa Kilimani.

Timu 20 zinatarajiwa kushiriki katika ligi hiyo ambayo itachezwa katika makundi mawili, kila kundi likiwa na klabu 10.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Issa Kassim alisema maandalizi yote ya kuelekea kuanza kwa ligi hiyo yamekamilika.

Kassim alisema tayari ukaguzi wa viwanja vitakavyotumika vya mikoa mitatu katika mechi za ligi hiyo ambayo itacheza kwa mtindo wa nyumbani na ugenini umekamilika.

"Tayari tumeshakagua viwanja vyote hasa katika Mkoa wa Kaskazini na Kusini, kwa upande wa Mkoa wa Mjini Magharibi tutatumia Uwanja wa Mau, viwanja ambavyo haviko katika ubora tumetoa maelekezo wafanye marekebisho kabla ya kuanza wa ligi," alisema Kassim.

# Nyumbu yaibana Polisi Tanzania FC

**Na Beatrice Shayo**

TIMU ya Nyumbu kutoka Pwani imetoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania inayoshiriki Ligi ya Championship katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Chuo Cha Polisi kilichoko Kurasini, Dar es Salaam juzi.

Nyumbu ambayo inajiandaa na msimu mpya wa First League mapema wiki hii ilitoka sare ya bao 1-1- dhidi ya Mashujaa kutoka Kigoma ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, mchezo uliofanyika kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Nyumbu, Rajab Gwamku alisema amefurahishwa na viwango vya wachezaji wake kupitia michezo hiyo ya kujipima nguvu waliocheza na wamepanga kuendelea kucheza mechi nyingine za kirafiki.

Gwamku amewaomba wadau wa soka wa Pwani kuiunga mkono timu yao ili ifanye vizuri katika msimu mpya na hatimaye kupanda daraja kushiriki Ligi ya Championship msimu ujao.

"Mchezo ulikuwa mzuri, timu ya Mashujaa na Polisi Fc zimeweza kutupa nguvu za kucheza vizuri zaidi katika mechi zetu zinazofuata, tumepata faida kupitia mechi hizi tulizocheza za kirafiki," Gwamku alisema .

## ZISIKUPITE

### MALEN ATAJWA LIVERPOOL

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp anavutiwa na winga wa Uholanzi, Donyell Malen mwenye umri wa miaka 24 baada ya kuanza vyema msimu huu akiwa na Borussia Dortmund. ***(Bild)***

### CHELSEA YAMTAKA OSIMHEN

CHELSEA inamfuatilia, Victor Osimhen wa Napoli na wako tayari kumnunua mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Nigeria mwenye umri wa miaka 24. (***Talksport***)

### OSIMHEN ANUKIA ARABUNI

KLABU ya K Al Hilal ya Saudi Arabia bado imeonyesha nia ya kumsajili, Victor Osimhen na itampa mkataba wa miaka mitano kwa pauni milioni 39 kwa mwaka na kukidhi bei ya Napoli inayotakiwa ya pauni milioni 173. (***Gazetta dello Sport***)

### HOJBJERG ATAJWA JUVE

KLABU ya Juventus imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 28 kutoka Tottenham Hotspur katika dirisha la Januari, lakini lazima wapunguze mchezaji wao mmoja kwanza ili kuokoa fedha. (***Calciomercato***)

### KLOPP AMTAKA ALCANTARA

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp anataka kuongeza mkataba wa kiungo wa kati wa Hispania, Thiago Alcantara, lakini wengine ndani ya Anfield hawana imani na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 32. (***90min***)

### CHELSEA, MAASTSEN BADO

HATIMA ya winga wa Uholanzi, Ian Maatsen katika klabu ya Chelsea bado haijaamuliwa na hakuna harakati zozote kuhusu mkataba mpya kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. (***Telegraph***)

### UNITED, CHELSEA VITANI

KLABU ya Manchester United na Chelsea zinavutiwa na kiungo wa Flamengo ya Brazil mwenye umri wa miaka 17, Lorran. ***(Express)***

### ZIDANE KUINOA MARSEILLE

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane (51), amekubali makubaliano na wawekezaji wa Saudi Arabia kutua Marseille iwapo watainunua klabu hiyo ya Ligue 1. (***Radio France Bleu Provence)***

### BRUCE KUTUA ICELAND

STEVEN Bruce mwenye umri wa miaka 62 anaweza kurejea katika usimamizi wa soka kama kocha mpya wa Jamhuri ya Ireland, huku shinikizo likiongezeka kwa kocha wa sasa, Stephen Kenny. (***The Sun)***

### ARSENAL, WHITE SAFI

KLABU ya Arsenal inatumaini kumpa mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia timu hiyo mlinzi wa England, Ben White mwenye umri wa miaka 25. (***Mirror***)

### JOELINTON MAMBO SAFI

MAZUNGUMZO kati ya Newcastle United na mshambuliaji wa Brazil, Joelinton mwenye miaka 27 kuhusu mkataba mpya yanaendelea vyema, huku Magpies hao pia wanataka kumwongezea mkataba beki wa Uholanzi, Sven Botman (23). (***The Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NAPOLI: HATUKUPANGA KUMKASHIFU OSIMHEN

**NAPLES,** Italia

●●●Ni kuhusiana na video iliyowekwa katika mtandao wa klabu baada...

NAPOLI imesema "hatukuwa na nia ya kumuudhi" Victor Osimhen baada ya klabu hiyo kutuma ujumbe kwenye mtandao wa kijamii wa TikTok ambao ulionekana kumkejeli mshambuliaji wao huyo nyota kwa kukosa penalti.

Video hiyo ambayo iliwekwa na kisha kufutwa kwenye TikTok rasmi ya Napoli Jumanne iliyopita na kufuatiwa na Osimhen akifuta takribani picha zake zote akiwa kwenye jezi ya timu hiyo katika akaunti zake za mitandao ya kijamii na wakala wake akisema anafikiria kuchukua hatua za kisheria.

"Ili kuepusha matumizi mabaya ya suala hilo, SSC Napoli ingependa kusema kwa uwazi klabu haikuwa na nia ya kumuudhi au kumdhihaki Victor Osimhen, ambaye ni mtu muhimu kwa klabu," ilisema taarifa ya Napoli jana.

"Katika kipindi cha majira ya joto, Napoli ilikataa ofa zote za kutaka kumsajili mshambuliaji huyo -- uthibitisho thabiti wa klabu hiyo kumthamini.

"Kwenye mitandao ya kijamii, na TikTok haswa, lugha ya kujieleza inatumika kwa njia nyepesi na ya kucheza. Katika kesi hii inayomhusisha Victor hapakuwa na nia ya dhihaka.

**"Ikiwa Victor alikasirishwa kwa njia yoyote, hii haikuwa kabisa nia ya klabu."**

Akizungumza baada ya ushindi wa mabao 4-1 wa Serie A Jumatano iliyopita dhidi ya Udinese, ambapo Osimhen alifunga bao, Kocha Mkuu wa Napoli, Rudi Garcia alisema jambo hilo "ugumu" lakini akaongeza mchezaji huyo amejitolea kuchezea mabingwa hao wa Italia.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria, Osimhen aliifungia Napoli mabao 31 msimu uliopita walipomaliza kusubiri kwa miongo mitatu kwa taji la Serie A na pia kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Licha ya mazungumzo juu ya mkataba mpya uliofunguliwa miezi iliyopita, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 bado hajasaini mkataba mpya, ambapo wa sasa unamalizika mwaka 2025.

"Ninaweza kukuhakikishia anaipenda jezi hii na anajitoa kwa hali na mali," alisema Garcia katika mahojiano baada ya mechi dhidi ya DAZN.

"Hakuna aliyetaka kufanya dhihaka, si TikTok wala Victor kwenye mitandao yao ya kijamii. Hakuna dhihaka iliyokusudiwa lakini kulikuwa na hisia za kukasilika.

Sijui kama sasa Osimhen atachapisha picha zake kwenye mitandao ya kijamii tena akiwa na jezi ya Napoli."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,157,29

MECHI KALI

YOUNG AFRICANS
VERSUS
AL-MERRIKH

1 | 1.15
X | 7.00
2 | 9.00

tigo pesa SportPesa

WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!

1. Ramfili Mkenda - 0654 829 XXX
2. Tizo Mbeyu - 0656 295 XXX
3. Jemaidi Kangarawe - 0659 582 XXX
4. Denis Kyando - 0673 519 XXX
5. Shaibu Mchoma - 0675 256 XXX
6. David David - 0678 244 XXX
7. Sarah Zakaria - 0679 602 XXX
8. Abdul Nzigilwa - 0711 745 XXX
9. Ally Rashidi - 0719 383 XXX
10. Ng'anzi Bakari - 0713 654 XXX

20,000/=
KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BARCA YATANGAZA FAIDA KWA MSIMU 2022/2023

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imetangaza kupata faida kubwa ya jumla euro milioni 304 kwa msimu wa 2022/2023.

Mapato ya jumla ya uendeshaji yalikuwa euro bilioni 1.259, wakati gharama za uendeshaji zilikuwa euro bilioni 1.165.

Katika mitiririko ya kibiashara (euro milioni 350) na uuzaji (euro milioni 100), Barcelona ilifurahia rekodi za mapato.

Mikataba ya ufadhili pia iliwawezesha kupata euro milioni 200, iliyoboreshwa kwa kusajili washirika 20 wapya.

Kama ilivyothibitishwa hapo awali, klabu ilichangisha euro milioni 400 kwa kuuza asilimia 15 ya haki za sauti kwa matangazo ya LaLiga.

Deni halisi limepungua tangu mwaka uliopita, sasa ni euro milioni 552 kutoka euro milioni 680.

Kushuka kwa deni la kumesababisha kushuka kwa deni la jumla la klabu hiyo.

Muhtasari kutoka katika klabu hiyo ulieleza: "Bodi imetathmini uwiano mzuri wa mwisho wa mwaka huu wa fedha, ambapo pia imeongeza hatua za kudhibiti na kupunguza matumizi ambayo yanatekelezwa tangu mwanzo wa mamlaka ya sasa mnamo mwaka 2021."

Rais wa Barca, Joan Laporta hivi majuzi alidai ahueni ya kifedha ya klabu hiyo, ambayo imewakatisha tamaa katika misimu ya hivi karibuni, itamaliza mapema kuliko ilivyotarajiwa.

"Tunaboresha katika nyanja zote," alisema.

"Sote tunadhani tuna kikosi kizuri sana mwaka huu, tunawapongeza wote wenye majukumu ya kimichezo, tumejitahidi sana kusajili wachezaji wote, tulioona watatufaa.

# Chelsea yamweka sokoni Cucurella



**LONDON,** England

CHELSEA iko tayari kusikiliza ofa kwa mlinzi wake, Marc Cucurella kuelekea dirisha dogo la usajili la Januari, kwa mujibu wa ESPN.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa pauni milioni 62 kutoka Brighton alicheza mechi yake ya pili msimu huu katika ushindi wa bao 1-0 wa raundi ya nne ya Kombe la Carabao dhidi ya klabu yake ya zamani, lakini bado hajacheza dakika hata moja kwenye Ligi Kuu England tangu, Mauricio Pochettino awe kocha mkuu.

Cucurella aliiambia ESPN katika mahojiano yake ya Julai, alitaka kubakia kwenye klabu hiyo na kupigania nafasi yake, lakini ukosefu wa dakika za kucheza katika miezi ijayo kutamlazimisha afikirie vinginevyo.

Chelsea walikuwa tayari kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ajiunge na Manchester United kwa mkopo msimu huu wa joto, lakini mpango huo ulishindikana baada ya Cucurella kucheza mechi ya awali ya klabu hiyo ya Kombe la Carabao dhidi ya AFC Wimbledon.

Kanuni za FIFA zinaeleza mchezaji hawezi kuwakilisha klabu tatu kwa msimu mmoja na hivyo mazungumzo hayo yalivunjika.

Ripoti kutoka Hispania zimehusisha na Real Madrid na uwezekano wa kuwasilisha ombi la mkopo Januari na matarajio ya kurejea katika nchi aliyozaliwa yanafikiriwa na Cucurella.

HABARI MICHEZO


# 90,273/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/09/23 | 19:30 | Tottenham Hotspur vs Liverpool FC | 2.80 | 3.90 | 2.15 |
| 02. 30/09/23 | 20:00 | Boavista Porto vs FC Famalicao | 2.17 | 3.30 | 3.15 |
| 03. 30/09/23 | 22:00 | Real Sociedad San Sebastian vs Athletic Bilbao | 2.21 | 3.15 | 3.25 |
| 04. 30/09/23 | 22:00 | AS Monaco vs Olympique Marseille | 2.20 | 3.65 | 2.85 |
| 05. 01/10/23 | 13:30 | Fatih Karagumruk Istanbul vs Kasimpasa Istanbul | 2.28 | 3.35 | 2.60 |
| 06. 01/10/23 | 14:30 | FC Nuremberg vs FC Magdeburg | 2.37 | 3.55 | 2.65 |
| 07. 01/10/23 | 14:30 | SV 07 Elversberg vs Greuther Furth | 2.50 | 3.60 | 2.48 |
| 08. 01/10/23 | 14:30 | VfL 1899 Osnabruck vs FC Kaiserslautern | 2.65 | 3.45 | 2.42 |
| 09. 01/10/23 | 16:00 | Nottingham Forest vs Brentford FC | 2.70 | 3.15 | 2.55 |
| 10. 01/10/23 | 16:00 | Udinese Calcio vs Genoa CFC | 2.08 | 3.20 | 3.45 |
| 11. 01/10/23 | 17:15 | Deportivo Alaves vs CA Osasuna | 2.55 | 3.00 | 2.80 |
| 12. 01/10/23 | 17:30 | FC Luzern vs FC Zurich | 2.24 | 3.25 | 2.70 |
| 13. 01/10/23 | 18:00 | FK Austria Wien vs SK Rapid Wien | 2.33 | 3.35 | 2.55 |
| 14. 01/10/23 | 18:00 | Hobro IK vs Kolding IF | 2.65 | 3.25 | 2.31 |
| 15. 01/10/23 | 19:00 | Konyaspor vs Besiktas Istanbul | 2.80 | 3.30 | 2.19 |
| 16. 01/10/23 | 19:00 | Viborg FF vs AGF Aarhus | 2.60 | 3.35 | 2.50 |
| 17. 01/10/23 | 19:00 | Atalanta BC vs Juventus Turin | 2.46 | 3.30 | 2.70 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 30/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 3717 | Aston Villa vs Brighton | 2.58 | 3.82 | 2.50 |
| 15:00 | 4725 | Getafe vs Villarreal | 2.88 | 3.19 | 2.56 |
| 16:00 | 1173 | Lecce vs Napoli | 4.62 | 3.75 | 1.77 |
| 16:00 | 2607 | Geita Gold FC vs KMC | 1.99 | 3.17 | 3.67 |
| 16:30 | 1935 | VfL Bochum vs Monchengladbach | 2.32 | 3.69 | 2.87 |
| 16:30 | 2498 | VfL Wolfsburg vs Eintracht Frankfurt | 2.14 | 3.49 | 3.39 |
| 16:30 | 2953 | Mainz vs Bayer Leverkusen | 5.11 | 4.40 | 1.60 |
| 16:30 | 3118 | FC Koln vs Stuttgart | 2.76 | 3.51 | 2.48 |
| 16:30 | 4527 | Heidenheim vs Union Berlin | 3.03 | 3.60 | 2.26 |
| 16:30 | 4533 | Rubin Kazan vs FC Krasnodar | 3.14 | 3.29 | 2.14 |
| 17:00 | 1396 | Norwich City vs Birmingham | 1.88 | 3.47 | 3.72 |
| 17:00 | 1433 | Manchester Utd vs Crystal Palace | 1.58 | 4.23 | 5.57 |
| 17:00 | 1669 | Bournemouth vs Arsenal | 5.57 | 4.64 | 1.53 |
| 17:00 | 2445 | Watford vs Middlesbrough | 2.25 | 3.31 | 2.91 |
| 17:00 | 2486 | Everton vs Luton Town | 1.60 | 3.91 | 5.97 |
| 17:00 | 2632 | Ross County vs Hearts | 3.08 | 3.43 | 2.14 |
| 17:00 | 2795 | Hibernian vs Dundee FC | 1.72 | 3.72 | 4.27 |
| 17:00 | 2885 | Rangers vs Aberdeen | 1.26 | 5.55 | 9.11 |
| 17:00 | 2914 | St Johnstone vs Livingston | 2.49 | 3.08 | 2.79 |
| 17:00 | 2974 | Bristol City vs Stoke City | 2.26 | 3.21 | 2.97 |
| 17:00 | 3557 | Millwall vs Swansea | 2.07 | 3.23 | 3.38 |
| 17:00 | 3655 | Shakhtar Donetsk vs Vorskla Poltava | 1.33 | 4.73 | 6.85 |
| 17:00 | 4096 | Kilmarnock vs St Mirren | 2.29 | 3.19 | 2.99 |
| 17:00 | 4967 | Newcastle vs Burnley | 1.34 | 5.55 | 8.22 |
| 17:00 | 5046 | Preston vs West Bromwich | 2.33 | 3.18 | 2.88 |
| 17:00 | 5204 | Ayr United vs Raith Rovers | 2.65 | 3.27 | 2.43 |
| 17:00 | 5431 | Cardiff vs Rotherham | 1.67 | 3.66 | 4.56 |
| 17:00 | 5491 | QPR vs Coventry | 2.93 | 3.23 | 2.28 |
| 17:00 | 5584 | Eupen vs Anderlecht | 3.99 | 3.84 | 1.74 |
| 17:00 | 5928 | West Ham vs Sheffield Utd | 1.47 | 4.64 | 6.39 |
| 17:15 | 5550 | Rayo Vallecano vs Mallorca | 2.19 | 3.13 | 3.64 |
| 18:00 | 3976 | Clermont Foot vs Paris St Germain | 5.97 | 4.44 | 1.52 |
| 19:00 | 2823 | Servette Geneva vs Lausanne-Sport | 1.90 | 3.51 | 3.66 |
| 19:00 | 3604 | Galatasaray vs Ankaragucu | 1.30 | 5.34 | 7.60 |
| 19:00 | 3823 | AC Milan vs Lazio | 1.84 | 3.50 | 4.54 |
| 19:00 | 4319 | Namungo vs Mashujaa FC | 1.75 | 3.30 | 4.25 |
| 19:00 | 4352 | Sparta Prague vs Viktoria Plzen | 1.74 | 3.83 | 4.09 |
| 19:00 | 4758 | Young Africans vs Al-Merrikh | 1.15 | 7.00 | 9.00 |
| 19:00 | 5458 | CSKA Moscow vs Baltika Kaliningrad | 1.63 | 3.70 | 4.83 |
| 19:15 | 3529 | OH Leuven vs Standard Liege | 2.23 | 3.59 | 2.79 |
| 19:30 | 1311 | RB Leipzig vs Bayern Munchen | 3.32 | 3.97 | 2.01 |
| 19:30 | 3078 | Girona vs Real Madrid | 3.54 | 3.85 | 1.97 |
| 19:30 | 3229 | Tottenham vs Liverpool | 2.85 | 3.84 | 2.28 |
| 19:30 | 4004 | Elche vs Levante | 2.22 | 3.18 | 3.08 |
| 21:30 | 2732 | Grasshoppers vs BSC Young Boys | 4.34 | 4.08 | 1.64 |
| 21:30 | 4218 | Farul Constanta vs Sepsi Osk | 2.10 | 3.19 | 3.34 |
| 21:45 | 2742 | Salernitana vs Inter | 6.99 | 4.73 | 1.44 |
| 22:00 | 1637 | Real Sociedad vs Athletic Bilbao | 2.25 | 3.20 | 3.41 |
| 22:00 | 2059 | Waalwick vs Ajax | 4.55 | 4.35 | 1.56 |
| 22:00 | 2460 | Monaco vs Marseille | 2.20 | 3.76 | 3.04 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# SIMBA YAPIGWA FAINI, YANGA YAPEWA ONYO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imepigwa faini ya Sh. milioni moja wakati watani zao, Yanga wamepewa onyo na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) kutokana na makosa ya kikanuni waliyofanya katika mechi zao zilizopita za ligi hiyo, imeelezwa.

Yanga imepewa onyo kali kwa kosa la kuwakilishwa pekee na Kocha Mkuu, Miguel Gamondi katika mkutano na waandishi wa habari kuelekea mechi yao dhidi ya JKT Tanzania uliopigwa Agosti 29, mwaka huu ambao walipata ushindi wa mabao 5-0.

Simba yenyewe imepigwa faini hiyo kwa kosa la baadhi ya maofisa wake wa usalama kumfanyia vurugu kiongozi mmoja wa Coastal Union katika mechi namba 22 iliyochezwa Septemba 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Katika mechi hiyo, Simba ilipata ushindi wa mabao 3-0.

Pia Simba imekutwa pia na kosa kama la Yanga la kumpeleka Kocha Mkuu, Roberto Oliveira 'Robertinho' peke yake katika mkutano na wanahabari kabla ya mechi hiyo bila kuambatana na nahodha au mchezaji mwenye ushawishi.

Uamuzi huo ulitolewa katika kikao kilichofanyika Septemba 27, mwaka huu ambacho kilipitia ripoti za michezo mbalimbali ya raundi ya tatu.

Katika taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi, uamuzi mwingine uliofanya na kamati hiyo ni kuipa onyo KMC kutokana na kuwakilishwa na maofisa wanne badala ya watano katika mkutano wa maandalizi, huku Kocha Mkuu, Abdihamid Moallin na mchezaji, Waziri Junior wakisababisha klabu hiyo ipate onyo lingine ya pili kwa kuchelewa kufika kwenye mkutano.

JKT Tanzania nayo imeangukia kwenye kosa kama hilo baada ya kuwakilishwa na Kocha Msaidizi, George Mketo, badala ya Kocha Mkuu, Malale Hamsini katika kikao cha maandalizi kuelekea mchezo huo dhidi ya Yanga.

Wakati huo huo Tabora United imepigwa faini ya Sh. milioni moja baada ya mashabiki wake kufanya vurugu kwenye mechi yao dhidi ya Prisons ikishinda mabao 3-1, pia kocha wa magolikipa wa Azam FC, Khalifa Aboubakar akitozwa faini ya Sh. 500,000 kwa kufanya vurugu katika mechi dhidi ya Singida Fountain Gate.




Gamondi Robertinho

## Simba, Power Dynamos zatishana Afrika

INATOKA UK 24

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally amesema wachezaji wao wako katika hatua ya mwisho ya kukamilisha maandalizi kuelekea mechi hiyo lakini wameonyesha wana hamu na mchezo wenyewe.

"Hali ya kikosi iko shwari na wachezaji wetu wanamzuka, wana hamu kubwa na mchezo wenyewe ili wakatimize lengo la kutinga makundi ambapo sisi kwetu Simba wala si habari kubwa sana kuingia hatua hiyo," alitamba Ahmed.

Wakati huo huo, kikosi cha Power Dynamos kilitua nchini juzi usiku kwa ajili ya mechi hiyo lakini bila kipa wake namba mmoja, Lawrence Mulenga ambaye aliumia na kukimbizwa hospitali katika mechi ya Ligi Kuu Zambia iliyochezwa Jumamosi iliyopita dhidi ya Zesco.

Kipa huyo alikuwa shubiri kwa wachezaji wa Simba kutokana na kuokoa mashambulizi mbalimbali yaliyoelekezwa katika lango lake na kuifanya mechi hiyo kumalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Katika mechi hiyo ya kesho Power Dynamos pia itamkosa beki wake wa kati tegemeo, Dominic Chanda ambaye alionyeshwa kadi nyekundu katika mchezo wa kwanza Levy Mwanawasa, Ndola Zambia kwa kumchezea vibaya, Baleke.

Meneja wa timu hiyo, Lombe Chipupu alisema hawana wasiwasi na mechi hiyo kwani wamekuja kushinda.

"Hatuna presha huu ni mpira, tumekuja kushinda, tunajua tupo hapa kwa sababu gani, tunajua tunahitaji kushinda au sare ya juu ya mabao 2-2 ndiyo matokeo yatakayotupeleka mbele, tumejipanga kwa hilo," alisema meneja huyo.

# Michezo

Jumamosi Septemba 30, 2023

Nipashe




Napoli: Hatukupanga kumkashifu Osimhen UK. 21



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Maxi Nzengeli (kulia), akiwania mpira dhidi ya beki, Attohoula Yao katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa kuwavaa Al Merrikh katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Simba, Dynamos zatishana Afrika

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba kimeendelea kujifua kuelekea mechi ya marudiano ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho dhidi ya Power Dynamos kwa Kocha Mkuu, Roberto Oliveira 'Robertinho' kuweka mkazo zaidi kwa wachezaji wake kuwa na shabaha wanapofika langoni.

Katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika juzi jioni kwenye Uwanja wa Mo Arena, Dar es Salaam, kulikuwa na idadi kubwa ya magoli madogo ambayo yalisambazwa uwanjani na Robertinho aliwataka wachezaji wake kupiga mipira kuelekea katika magoli hayo.

Mazoezi hayo yameonyesha wazi hataki makosa yaliyofanyika katika mechi ya kwanza iliyochezwa Septemba 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa, Ndola yanajirudia kwa wachezaji wakiongozwa na straika, Jean Baleke kukosa mabao mengi ya wazi.

"Kila kocha ana mbinu zake za ufundishaji kila siku, huwezi kufundisha vilevile kila siku, mara nyingi mwalimu bora ni yule anayetengeneza aina tofauti tofauti ya ufundishaji na mbinu kutokana na mapungufu yanayojitokeza na aina ya mpinzani unayekwenda kucheza naye," alisema Robertinho.

INAENDELEA UK 23

# Yanga kamili kuvunja rekodi

## Haijacheza makundi Afrika kwa miaka 25, serikali yaomba...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI Yanga inawakaribisha Al Merrikh kutoka Sudan katika mechi ya marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku ikisaka rekodi muhimu, serikali imewaomba mashabiki wa soka nchini kuziunga mkono timu zote za taifa, imeelezwa.

Yanga inakutana na Al Merrikh ikiwa inahitaji kuvunja rekodi ya kutoshiriki hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa miaka 25, mara ya mwisho wawakilishi hao walicheza hatua hiyo mwaka 1998.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara leo watawavaa Al Merrikh wakiwa na faida ya ushindi wa mabao 2-0 walioupata katika mechi ya kwanza iliyochezwa Kigali, Rwanda.

Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi alisema maandalizi ya kikosi chake yamekamilika na wachezaji wako tayari kumalizia dakika 90 za mwisho kwa kusaka ushindi na kufanikiwa kutinga makundi.

Gamondi alisema amewaandaa vyema vijana wake kimwili na kiakili kwa ajili ya kutafuta ushindi na amewaambia wasahau matokeo ya mechi ya kwanza na kujipanga kuanza upya.

"Tumefanya maandalizi mazuri na wachezaji wote wako tayari, haitakuwa mechi rahisi kwa sababu Al Merrikh watakuja kivingine, tunatakiwa kuongeza umakini ili kutafuta ushindi ambao utatusaidia kusonga mbele na kuchezа hatua ya makundi," alisema Gamondi.

**Aliongeza endapo kila mchezaji atafuata vizuri maelekezo yake, watapata ushindi na hatimaye watatimiza malengo ya klabu.**

Naye Kocha Mkuu wa Al Merrikh, Osama Nabieh alisema itakuwa mechi nzuri na yenye ushindani mkubwa kwa sababu wanahitaji kupata ushindi wa mabao 3-0 ili wasonge mbele katika mashindano hayo.

Nabieh alisema licha ya kupoteza mechi ya kwanza, bado mechi hiyo haijaisha na wanatambua Yanga ni timu nzuri na imara lakini wako nchini kwa ajili ya kupambana katika mchezo huo.

"Tunawaheshimu Yanga, hautakuwa mchezo rahisi, tunahitaji kushinda, tunatambua ubora wao lakini tumekuja Tanzania kwa ajili ya kupambana na kupata ushindi mkubwa na kusonga hatua ya makundi," alisema Nabieh.

Aliongeza hawataathirika na presha ya makelele ya mashabiki wa Yanga watakaokuwepo uwanjani kwa sababu amewahi kucheza na timu kubwa Afrika zikiwa na mashabiki wengi ikiwamo Zamalek.

Nyota wa timu hiyo, Bakhit Khamis alisema kazi kubwa iliyopo mbele yao ni kutafuta ushindi katika mechi hiyo ili kufikia malengo.

Khamis alisema Yanga walitumia vizuri makosa waliyofanya katika mechi ya kwanza na kupata ushindi, lakini kwa sasa wamejiandaa vizuri kupambana na tayari wamerekebisha mapungufu yao kwa sababu wanahitaji kufikia malengo kwa kuwatoa wapinzani wao.

"Kazi kubwa imebaki kwetu, tunatambua ubora wa Yanga, tunaenda kupambana kwa ajili ya kusaka ushindi na kupita hatua ya makundi," alisema mchezaji huyo.

Naye, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro amesema huu ni wakati wa Watanzania kuwa kitu kimoja kwa kuziunga mkono timu zetu kama sehemu ya maandalizi ya kuelekea fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

Ndumbaro alisema kujitokeza idadi kubwa ya mashabiki viwanjani ndio hamasa na kigezo cha Tanzania kupata fursa ya kucheza mechi ya ufunguzi au fainali.

"Hamasa ya mpira wa Yanga na Simba imekuwa kubwa na ndio sababu Shirikisho la Soka Afrika (CAF ), wameweka mechi ya ufunguzi ya 'Super League' kwa kuzikutanisha timu za Simba na Al Ahly mchezo utakaochezwa Oktoba 20, mwaka huu kwenye Uwanja waBenjamin Mkapa," alisema Ndumbaro.

Waziri huyo pia amezitaka Simba na Yanga zisibweteke na matokeo waliyoyapata kwenye mechi zao za kimataifa zilizopita na badala yake ziongeze juhudi zaidi kuelekea mechi za marudiano.

Pia amezitaka sekta binafsi kuhakikisha zinachangamkia fursa pindi timu zitakapoanza kuwasili hapa nchini kwa sababu zitahitaji chakula, malazi na usafiri.

"Safari bado haijaisha tuna mechi mbili za nyumbani na ugenini dhidi ya Togo, hii ni muhimu kwa kuwa tunaimani tutafuzu WAFCON na huku tunataka baada ya kupata nafasi AFCON 2027," Ndumbaro alisema.

Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia alisema matayarisho ya Taifa Stars yameanza kwa kuwasilisha mapendekezo muhimu ili timu hiyo ifanye vizuri.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >